# NAFASI YA FASIHI KATIKA KUWASILISHA MASUALA YA MAZINGIRA KUPITIA RIWAYA TEULE *TIKITIMAJI (2013)* NA *MSIMU WA VIPEPEO (2006)* ZA K.W WAMITILA

**WESONGA LUCY ESTHER**

**TASNIFU YA UTAFITI ILIYOWASILISHWA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA MOUNT KENYA**

**OCTOBA, 2021**

## UNGAMO

**UNGAMO LA MWANAFUNZI**

"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya shughuli yoyote ile wala kwa minajali ya shughuli ile wala kwa mahitaji ya shahada katika chou chochote"

Sahihi ______________ Tarehe 1/1/2021

WESONGA LUCY ESTHER

MAKI/2014/72016

**UNGAMO LA WASIMAMIZI**

Uandishi wa kazi hii umeelekezwa na wasimamizi wa chuo kikuu cha Mount Kenya wafuatao:

Sahihi ______________ Tarehe 03rd.04.2021

DKT ASIKO BEVERLYNE AMBUYO

Mhadhiri Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Maseno

Sahaihi ______________ Tahehe 23.04.2021

PROFESA ROCHA MZUNGU CHIMERAH

Mhadhiri Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Pwani

## TABARUKU

Kazi hii naitabarukia mama mzazi Josphine Egesa Kwa kunielimisha na kunihimiza. Mungu amzidishie miaka mingi humu duniani.

## SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu mwenye rehema zote kunifikisha hapa. Kufanikiwa na kukamilika kwa kazi hii kumetokana na jitihada za watu wengi. Kwa mintarafu hii, ningependa kuwashukuru wafuatao:

Kwanza natoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu, daktari Asiko Beverlyne Ambuyo na profesa Rocha Chimerah kwa kunielekeza na kuniongoza kuihakiki kazi hii, mchango wenu ulinifaa sana. Nawashukuru wanafunzi wenzangu wa chuo kikuu cha Mount Kenya kwenye idara ya Kiswahili kwa ushauri wenu mwafaka.

Nawashukuru wanangu, Ryan, Austine na Anwyll kwa stahamala kuu nilipokuwa nimezama kwenye kazi hii. Kwa watoto wangu najifunga kibwebwe ili niwe kielelezo bora kwenu. Pia, nawashukuru dada zangu, Jane, phemina, Blacky Jemima na kaka yangu Isaac kwa ushauri wenu na kunitia moyo mambo yaliponizidia. Nakiri “Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe. Sitachelea kuwashukuru marafiki wangu Winnie na Oketch kwa ushauri wenu ulioniwezesha kuvuka bahari hii.

# IKISIRI

Suala la mabadiliko ya hali ya anga ni janga linaloendelea kukumba ulimwengu kwa jumla. Kutokuwepo kwa usawazishaji wa ikolojia ni jambo ambalo linawatia shaka adinasi wengi. Fasihi ni kioo cha jamii na inapaswa kuwasilisha hali halisi ya maisha ya binadamu. Utafiti huu ulichambua nafasi ya fasihi katika kuwasilisha masuala ya mazingira kupitia riwaya mbili teule za wamitila, *Tikitimaji* (2013) na *Msimu Wa Vipepeo* (2006). Niliteua riwaya za Wamitila kwa sababu mwandishi huyu ameonyesha ari katika uwanja wa fasihi mazingira, kwenye makala yake ya *"place and placelessness in Kiswahili literature: The role of setting in Kiswahili creative writing*" (1999), anasema kuwa mandhari huchukua nafasi katika kuwasilisha masuala ya mazingira. Hivyo utafiti ulichunguza namna alivyotumia fasihi kuwasilisha masuala ya mazingira katika riwaya zake. Ingawa kwa miaka mingi, masuala ya mazingira yamehusishwa na sayansi haswa katika kutoa takwimu kamilifu kuhusiana na masuala ya mazingira, fasihi inaendelea kuchukua dhima mpya katika jamii inayozidi kukua kiteknolojia. Utafiti huu uliongozwa na madhumuni yafuatayo: kubainisha jinsi mwandishi wa riwaya ya Tikitimaji alivyotumia wahusika ili kuwasilisha maudhui ya mazingira; pili, kueleza mitindo ya lugha iliyotumiwa kuwasilisha masuala ya mazingira na tatu, kutathimini iwapo mwandishi amefaulu kuwasilisha maudhui ya mazingira riwayani. Utafiti huu ulitumia kiunzi cha nadharia kutoka kwa nadharia ya fasihi mazingira na nadharia ya uhalisia. Mihimili zilizotumiwa kutoka kwa nadharia ya uhalisia ni: kazi ya fasihi imejitosheleza, kazi ya msanii inapaswa kuwasilisha ukweli, mtunzi anaangalia matatizo na kuchunguza chanzo chake na mwisho wahusika ni vielelezo yakini vya binadamu wa kawaida kwa vile wao hutumia lugha ya kawaida wanayoitumia humwezesha mwanadamu kujifafanulia uwezo wake wa kutenda mambo. Kutoka kwa nadharia ya fasihi mazingira, mihimili ifuatayo ilitumika: fasihi inapaswa kuwasilisha mielekeo ya binadamu kuhusu mazingira, kuangalia matumizi ya dhana za ekolojia katika kazi za kifasihi, nguvu za kibinadamu na lugha ya binadamu kuhusiana na mazingira, huangalia mitindo ya lugha na jinsi mitindo hiyo huathiri namna binadamu anavyotagusana na mazingira na mwisho huchukulia kuwa mazingira na utamaduni hushirikiana katika ujenzi wa lugha na fasihi, binadamu hawezi kuishi bila ekolojia lakini ekolojia huweza kuishi bila binadamu pia huangalia jinsi waandishi huwakilisha masuala ya mazingira na jinsi kazi hiyo huathiri mielekeo ya ulimwengu katika hali halisi. Muundo wa utafiti ulikuwa ni wa kiuchanganuzi. Utafiti ulifanywa maktabani. Riwaya za Wamitila, *Tikitimaji* (2013) na *Msimu Wavipepeo* (2006) ndizo zilizoteuliwa kimakusudi kama sampuli ya utafiti huu. Data ilipangwa kwenye makundi na kuchanganuliwa kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti na mihimili ya kiunzi cha nadharia. Data iliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Utafiti huu ulilenga kuhamasisha wasomi na waandishi wa fasihi wajikite zaidi kulenga masuala ya mazingira ambayo ndicho kitovu cha maisha ya binadamu. Utafiti ulibaini kuwa fasihi ni nyenzo mwafaka ya kuwasilisha masuala ya mazingira kupitia vipengele vyake. Hii ni kwa sababu fasihi huingiliana sana na utamaduni wa jamii.

## ABSTRACT

The issue of climatic change continues to worry all humanbeings at large. Lack of ecological balance worries human beings. Literature is the mirror of society and it is supposed to present real issues affecting humanity. The research was carried out to analyse the role of literature in presenting environmental issues through two selected Kiswahili novels: *Tikitimaji (*2013) and *Msimu Wa Vipepeo* (2006), written by Wamitila. We chose Wamitilas' novels because in his article titled *place and placelessness in Kiswahili literature:The role of setting in Kiswahili creative writing* (1999), he shows interest in the field of ecocriticism whereby he says that one should read the environment through setting. I chose his recently written novels to see how he has used literature to present environmental issues. Although for many years, environmental issues have been closely associated with sciences, literature continues to take up new roles in the society that continues to grow in terms of technology. The research had three objectives: one, to analyse how the author used characters in his novels to portray the theme of environment, two, to explain the language and the stylistic devices employed by the author to present the theme of environment in the novels and lastly, to examine whether the author succeeded in presenting environmental issues in the novels: Tikitimaji (2013) and *Msimu Wa Vipepeo* (2006). The research was guided by realism theory and ecocriticism theory. The following tenets from realism theory were used: The work of literature is independent, the writers' piece of work is supposed to say the truth, the writer looks at the problems and makes an analysis of their source and lastly, characters are real representations of humanbeings who use the language understood by humanbeings that makes them to act. From ecocriticism theory the following principles were used: literature is supposed to present humanbeings' attitudes towards the environment, ecocritical writing looks at ecological concepts in the works of literature, ecological writing should focus on human energy towards environment and lastly, the language and the stylistic devices used should show how humanbeings interact with environment and culture, . The research design was analytical. The research was carried out in the library. Purposive sampling was done whereby we arrived at two novels written by .Wamitila which tackled environmental issues. The tool for data collection was an observation checklist, data analysis was through content analysis while data presentation was through the explanation method. The research was carried out to motivate literature writers to focus more on ecological issues since man cannot stay without the ecology. The research found out that literature is agood device through which environmental isssues should be presented. This is because literature is closely connected to human culture.

## FAHARASA


**UNGAMO** .......... **ii**

**TABARUKU** .......... **iii**

**SHUKRANI** .......... **iv**

**IKISIRI** .......... **v**

**ABSTRACT** .......... **vi**

**FAHARASA** .......... **vii**

**ORODHA YA VIFUPISHO** .......... **xi**

**SURA YA KWANZA** .......... **0**

**UTANGULIZI** .......... **0**

1.0 Utangulizi .......... 0

1.1 Usuli wa Utafiti .......... 0

1.2 Suala la utafiti .......... 4

1.3 Madhumuni ya utafiti .......... 4

1.4 Nadharia tete .......... 5

1.5 Sababu za kuteua mada .......... 5

1.6 Upeo na mipaka .......... 6

1.7 UFAFANUZI WA ISTILAHI .......... 9

**SURA YA PILI** .......... **10**

**MISINGI YA KINADHARIA** .......... **10**

2.0 Utangulizi .......... 10

2.1 Yaliyoandikwa kuhusu mada .......... 10

2.1.1 Fasihi mazingira .......... 10

2.1.2 Matumizi ya mtindo katika kuwasilisha maudhui .......... 14

2.1.3 Matumizi ya wahusika katika kuwasilisha maudhui .......... 16

2.2 Kiunzi cha nadharia ........ 18

2.3 Hitimisho ........ 22

**SURA YA TATU ........ 23**

**NJIA NA MBINU ZA UTAFITI ........ 23**

3.0 Utangulizi ........ 23

3.1 Muundo wa utafiti ........ 23

3.2 Eneo la utafiti ........ 23

3.3 Kundi lengwa ........ 23

3.4 Usampulishaji ........ 24

3.6 Uchanganuzi wa data. ........ 25

3.7 Uhalali wa data. ........ 25

3.8 Kuaminika kwa kifaa cha kukusanyia data ........ 25

3.9 Uwasilishaji wa matokeo ya utafiti ........ 26

3.9.1 Maadili ya utafiti ........ 26

3.9.2 Hitimisho ........ 26

**SURA YA NNE ........ 27**

**UCHANGANUZI WA WAHUSIKA NA LUGHA KITAMATHALI NA JINSI ILIVYOKUZA MAUDHUI YA MAZINGIRA ........ 27**

4.0 Utangulizi ........ 27

4.1 Usawiri Wa Wahusika Katika Kuwasilisha Maudhui Ya Mazingira ........ 27

4.1.1 Dhana ya uhusika ........ 27

4.1.2 Uainishaji wa wahusika ........ 28

4.1.3 Njia nyingine za kusawiri wahusika ........ 29

4.2 Wahusika katika riwaya ya Tikitimaji ........ 30

4.2.1 Zinji, Kombo, Maya na Sapna kama vielelezo wa uzinduzi wa mazingira. ...............30

4.2.2 Mzee Jududi ....................................................................................................35

4.2.3 Mzee Dhamiri ..................................................................................................36

4.2.5 Jitikti ..............................................................................................................38

4.3 Usawiri wa Wahusika Katika Kuwasilisha Maudhui Ya Mazingira Katika Riwaya ya Msimu wa Vipepeo ...............................................................................38

4.3.1 Mkurutu kama waziri wa utalii na mazingira ..................................................38

4.3.3 Kalulu.............................................................................................................41

4.5.4 Guttasu Berlusconi..........................................................................................42

4.3.4 Mzee Kitali .....................................................................................................43

*4.3.5* Fabio Mkalla ...................................................................................................43

4.4 Uchanganuzi wa lugha kitamathali Katika Riwaya Ya Tikitimaji katika kuwasilisha masula ya mazingira ...........................................................................44

4.4.1 Matumizi ya tashibihi .......................................................................................44

4.4.2 Methali ............................................................................................................47

4.4.3 Tashihisi/uhaishaji ..........................................................................................51

4.4.6 Misemo ...........................................................................................................56

4.4.7 Takriri .............................................................................................................57

4.5 Matumizi Ya Lugha Katika kuwasilsha masuala ya mazingira katika Riwaya Ya Msimu Wa Vipepeo ...........................................................................................59

4.5.1 Mbinu Rejeshi..................................................................................................59

4.5.2 Nidaa...............................................................................................................60

4.5.3 Uhaishaji ........ 61

4.5.5 Tashibihi ........ 62

4.5.6 Mandhari ........ 63

4.6 Kumtathimini mwandishi ........ 63

4.6.1 Hitimisho ........ 67

**SURA YA TANO ........ 69**

**MUHTASARI, MATOKEO YA UTAFITI NA MAPENDEKEZO ........ 69**

5.0 Utangulizi ........ 69

5.1 Kuhusu madhumuni ya utafiti ........ 69

5.3 Mapendekezo kuhusu utafiti zaidi ........ 73

**MAREJELEO ........ 74**

**VIAMBATANISHO ........ 79**

KIAMBATANISHO I: ORODHA YA UCHUNZAJI ........ 79

KIAMBATANISHO II: BARUA YA SHULE ........ 80

KIAMBATANISHO III: BARUA KUTOKA KWA ERC ........ 81

KIAMBATANISHO IV: KIBALI CHA UTAFITI ........ 82

KIAMBATANISHO V: ITHIBATI KUTOKA NACOSTI ........ 83

KIAMBATANISHO V: BARUA KUTOKA KWA WIZARA YA ELIMU ........ 84

KIAMBATANISHO VI: BARUA KUTOKA KWA SERIKALI ........ 85

PLAGIARISM REPORT ........ 86

## ORODHA YA VIFUPISHO

Dkt.  Daktari

Kt.  Kisha tajwa

UNFCC.  United Nations Framework Convention on Climate change

Bw.   Bwana

IPCC. Intergovernmental Panel on Climate Change

OCHA. Office for the Coordination of Humanitarian Affairs

UN. United Nations

UNCED. United Nations Conference on Environment and Development

UK. Ukurasa

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Utangulizi

Katika sura hii utafiti ulishughulikia usuli wa utafiti, suala la utafiti, madhumuni yaliyoongoza utafiti, nadharia tete, sababu za kuteua mada, upeo na mipaka ya utafiti huku sura hii ikikamilika na ufafanuzi wa isitilahi kama zilivyotumika katika utafiti huu.

## 1.1 Usuli wa Utafiti

Utafiti huu ulichunguza nafasi ya fasihi katika kuwasilisha masuala ya mazingira kupitia riwaya teule ya *Tikitimaji* (2013) na *Msimu Wa Vipepeo* (2006) zake Wamitila. Fasihi ni sanaa inayotumia lugha na ambayo hujishughulisha na maisha ya binadamu na huathiri, hugusa au huacha athari fulani inayopatikana katika umbo ambalo linatambuliwa na jamii (Wamitila, 2004). Williady (2015), anasema kuwa fasihi ni tawi mojawapo la sanaa linalotumia lugha katika kuwasilisha ujumbe kwa njia ya maandishi au mdomo. Kwa mujibu wa waandishi hawa, fasihi imefasiriwa kama tawi la sanaa ambalo huwasilisha ujumbe fulani kwa jamii kwa kutumia lugha. Nao Njogu na Chimerah (1999), wanaeleza kuwa fasihi inawasilisha hali, maingiliano na mikinzano miongoni mwa binadamu na mazingira.

Fasihi huwasilisha maudhui yenye mguso kwa wanajamii kupitia kwa lugha ya mvuto. Wakiendelea, (Njogu na Chimera kt) wanasema kuwa msanii ni zao la jamii katika uhalisia wake. Msanii huchota maudhui yake kutokana na hali halisi zinazomzunguka za kitamaduni, kijamii na kisiasa. Mwandishi wa kazi za fasihi husimulia tajriba mbalimbali ambazo zimemkumba au kugusia jamii. Hakuna fasihi inayotokea kwenye ombwe tupu, kila fasihi ni zao la jamii. Fasihi huchukua nafasi kubwa katika jamii. Achebe (1988), anasema kuwa fasihi iwe imeandikwa au imerithishwa kwa njia ya

mdomo hutupa nafasi ya kuwasilisha ukweli. Achebe anaamini kuwa fasihi huwa na jukumu la kijamii na la kisiasa. Fasihi ni zaidi ya mapambo tu. Hutupa tajriba ya kila siku ya maisha, hutuelimisha kuhusu maana ya matendo yetu, hutuburudisha na kutudhibiti kimaisha. Fasihi hufanya kazi kwa kutuwezesha kukabiliana na majanga ya maisha na wakati uo huo ikitupa maarifa ya kujitambua na kusuluhisha majanga hayo ya ulimwengu kwa jumla.

Ekolojia yetu imo katika hali ya hatari ya maangamizi kutokana na matendo ya kibinafsi ya kibinadamu (IPCC, 2013). Matendo kama vile; ukataji wa miti, ujenzi wa nyumba katika maeneo oevu, ongezeko la teknolojia haribifu na ukosefu wa uongozi adilifu. Mwisho wa matukio haya ni kwamba kuna ongezeko la joto hewa na kuvugutwa kwa sayari, magonjwa, vifo na kupungua kwa mazao hali inayopelekea makali ya njaa. Walace (2001), anasema kuwa mazingira hayarejelei tu mazingira asilia bali pia huhusisha mandhari yaliyojengwa na binadamu pamoja na mitagusano ya elementi hizo asilia na utamaduni.

Utata huu umewasilishwa na idadi kubwa ya ripoti na makongamano mbalimbali yanayoangazia majanga ya kimazingira. Ripoti ya UN ya *Office for the Coordination of Humanitarian Affairs* (OCHA) (2015, mkutano wa dharura), inasema kuwa majanga ya tabianchi yanazidi kuongezeka. Shirika la umoja wa kimataifa kuhusu mazingira na maendeleo (UNCED) lililofanyika Rio de Jeneiro June 14 (1992) linalojulikana kama ajenda 21 lilikuwa na madhumuni ya kusitisha athari za kimazingira zinazotokana na kudorora kwa mazingira. Pia juhudi hizi za uhifadhi wa mazingira zinabainishwa na Wangari Mathai (1977) alipozindua muungano wa *Green Belt movement* akihusisha wanawake katika upandaji wa miti.

Canter (1975), anabainisha aina za uchafuzi wa mazingira katika makundi manne; uchafuzi wa hewa, uchafuzi wa maji, uchafuzi wa kelele na uchafuzi wa biolojia.

Kulingana na ripoti ya *Intergovernmental Panel on Climatic Change* (IPCC) (2014)) ambayo ilihusisha makundi matatu, inasema kuwa miongo miwili ya karne ya ishirini ilikuwa yenye ongezeko la joto hewa. Hali hii inachangiwa na athari chafu ya hewa, ukataji miti hali ambayo imepunguza gesi ya kaboni diooksidi. Pia athari hii ya uchafuzi wa mazingira inathibitishwa na Okpong (1994) anayeshadidia kuwa baadhi ya magonjwa ya ngozi na upungufu wa mazao mashambani yamesababishwa na miale mikali ya jua.

Majanga haya ya kimazingira hukumba kila mwanajamii bila kubagua maeneo wanamopatikana. Maamuzi yetu Kuhusiana na uchafuzi wa mazingira ndio hutofautiana. Kwa mujibu wa Reuveny (2007), anasema kuwa watu huweza kuliangalia suala la uchafuzi wa mazingira kwa njia tatu: Kwanza, wanaweza kukaa mahali pale pachafu bila kufanya chochote, Pili, Binadamu wanaweza kuzikubali changamoto za majanga ya kimazingira na mwisho, wanaweza kuamua kuleta mabadiliko katika sehemu zilizoathirika.

Maamuzi haya kuhusiana na masuala ya kimazingira, humotishwa na ufahamu wa kuhamasishwa kwa wanajamii kuhusiana na suala hili. Fasihi ni nyenzo mmojawapo muhimu yenye kuleta mahamasisho hayo. Kama asemavyo Vasquez (1983): Kazi ya sanaa huathiri watu na inachangia katika kuhimiza au kupuuza dhana zao, maazimio yao na hata maadili yao, yana msukumo wa kijamii ambao huathiri watu kwa nguvu zake za kihisia na kiitikadi. Chembilecho Vasquez (1983) fasihi huchukua nafasi kubwa sana katika kukuza maadili na mielekeo ya wanadamu kuhusiana na masuala fulani katika jamii. Ingawa mashirika ya kimazingira yamejihusisha sana na masuala ya mazingira katika viwango vya kitaifa na kimataifa, je, Fasihi inahusika vipi katika kuwasilisha masuala yaya haya?

Garrard (2007), anaeleza kwamba matatizo ya kimazingira yanaonekana kimsingi kuwa matatizo ya kisayansi na mijadala mingi kuhusu ongezeko la joto hewa huhusisha zaidi wanaangahewa kuliko watunzi wa ushairi au hata wahakiki wa fasihi. Kutokana na mwelekeo wake, masuala haya ya kimazingira yaweze kuwasilishwa kwa jamii kupitia fasihi kwani fasihi ndiyo huingiliana pakubwa na utamaduni wa jamii, na hivyo itaweza kuwafikia moja kwa moja.

Ni kutokana na kauli hii ya Garrard ndipo utafiti wetu ukajiegemeza kubaini jinsi mwandishi wa riwaya hizi mbili, *Tikitimaji* (2013) na riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* (2007) anavyowasilisha maudhui haya. Wamitilia (1999), katika makala yake ya *Place and placelessness in Kiswahili literature: The role of setting in Kiswahilili creative writing*, anaangalia nafasi ya mandhari katika kuwasilisha masuala ya mazingira katika riwaya ambapo anasema kuwa mandhari huweza kutumika kuelezea hali ya mazingira ijayo. Anaonyesha ari katika uwanja huu wa fasihi mazingira ndiposa tunachambua riwaya zake ili kutathmini jinsi anavyowasilisha masuala haya ya mazingira. Anasema kuwa inapaswa mtu kusoma mazingira kupitia mandhari. Kwake, mandhari hutaabiri hali ya mazingira yajayo. Ni muhimu suala la mazingira kuangaliwa kwa jicho pevu kwani binadamu wanapoharibu mazingira, utamaduni wao husambaratika. Kama asemavyo Ngugi (1995) msingi wa jamii ya binadamu ni ardhi, bila ardhi hamna jamii. Ngugi anaiona fasihi kama ung'amuzi wa mtunzi katika viwango vya kibinafsi na kijamii. Maoni yake Ngugi (1995) ni mkabala sawa na Unerchesky (1973) anayebaini kuwa ni muhimu fasihi ipongeze watu kwa mchango wao wanaofanya katika jamii. Watunzi wa fasihi kwa jumla wana jukumu la kuwaonyesha wanajamii matukio katika mazingira yao.

Fasihi nayo, kwa upande mwingine, huakisi mazingira ya kijamii. Jinsi mazingira yanavyobadilika ndivyo fasihi inaendelea kuchukua dhima ya uchunguzi wa jamii huku

ikibeba silaha mpya za utunzi, fikra za majadiliano na pia ikijihusisha na matatizo ya jamii mpya (Gromov, 2004). Katika kazi hizi za fasihi wahusika, mitindo na maudhui, hutumiwa kuwasilisha uhalisia wa kijamii. Suala la mazingira ni suala la kijamii na hivyo lapaswa kuangaziwa kwa undani kwani linapojitokeza katika fasihi huwasilisha maoni ya wanajamii. Walace (2001), anasema kuwa mazingira hayarejelei tu mazingira asilia bali pia huhusisha mandhari yaliyojengwa na binadamu pamoja na mitagusano ya elementi hizo asilia na utamaduni.

**1.2 Suala la utafiti**

Utafiti huu ulinuia kuchunguza nafasi ya fasihi katika kuwasilisha masuala ya mazingira katika riwaya ya *Tikitimaji* (2013) na riwaya ya *Msimu Wa Vipepeo* (2007). Utafiti huu ulichochewa na ukweli kwamba fasihi huingiliana sana na utamaduni wa jamii ya binadamu. Fasihi ni kioo cha jamii yetu, inaelimisha, inafundisha na kuzindua jamii. Inafaa kuteua maudhui yenye mguso kwa jamii na kuyasimulia kwa kiwango cha juu cha umbuji. Majanga ya mazingira yanaendelea kuongezeka hata kama yanawekwa wazi na takwimu za kisayansi. Kama asemavyo Wafula na Njogu (2007), fasihi ni usanii ambao hauwezi kujitenga na mazingira, msanii mara nyingi huzoa malighafi yake ya sanaa katika jamii yake, lengo lake likiwa ni kuarifu kuhusu ulimwengu na jamii kwa jumla.

**1.3 Madhumuni ya utafiti**

Utafiti huu utaongozwa na lengo kuu ambalo ni kutathmini nafasi ya fasihi katika kuwasilisha masuala ya mazingira kwa madhumuni yafuatayo:

a) Kubainisha jinsi Wamitila anavyotumia wahusika katika kuwasilisha maudhui ya mazingira katika riwaya za *Tikitimaji* (2013) na riwaya ya *Msimu Wa Vipepeo* (2006).

b) Kuchanganua namna mitindo ya lugha ilivyotumiwa kuwasilisha masuala ya mazingira katika riwaya ya *Tikitimaji (2013)* na *Msimu Wa Vipepeo* (2006).

c) Kutathimini iwapo mwandishi wa riwaya ya *Tikitimaji* (2013*) na Msimu Wa Vipepeo* (2006*)* amefaulu kuwasilisha maudhui ya mazingira riwayani.

**1.4 Nadharia tete**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tete zifuatazo:

a) Wamitila amewatumia wahusika katika kuwasilisha maudhui ya mazingira.

b) Mitindo ya lugha imetumiwa kuwasilisha masuala ya mazingira katika riwaya ya Tikitimaji na Msimu Wa Vipepeo.

c) Mwandishi wa riwaya ya Tikitimaji na Msimu Wa vipepeo amefaulu kuwasilisha maudhui ya mazingira riwayani.

**1.5 Sababu za kuteua mada**

Utafiti huu umechochewa na sababu zifuatazo:

Mwandishi Wamitila anaonyesha ari katika uwanja wa fasihi mazingira kupitia makala yake ya (1999) yenye mada ya *Place and placelessness in Kiswahili literature: The role of setting in Kiswahili creative writing*. Utafiti huu ulitaka kubainisha ni kwa jinsi gani mwandishi huyo amewasilisha masuala ya mazingira. Kwake anasema kuwa inampasa mja kusoma mazingira kupitia mandhari. Utafiti ulinuia kutathimini jinsi mwandishi Wamitila alivyowasilisha masuala ya mazingira kupitia riwaya zake mbili teule *Tikitimaji* (2013) *na Msimu Wa Vipepeo* (2007) Tulinuia kueleza jinsi mwandishi alivyowasilisha masuala ya mazingira kupitia riwaya zake teule.

Utafiti wa awali uliopo katika uwanja wa fasihi mazingira umeangazia jinsi fasihi inavyoweza kutumiwa kuhifadhi mazingira kupitia nyimbo; Sangili (2012) katika makala yake ya *Shifting towards East African ecological criticism in oral literature: An ecoanalysis of Maragoli songs*, anaegemea sana fasihi simulizi kuonyesha jinsi nyimbo

za Kimaragoli za kijani kibichi zinavyotumiwa kuhamasisha wanajamii kuhifadhi mazingira. Utafiti huu ulinuia kuwasilisha masuala ya mazingira kupitia fasihi andishi hususan riwaya.

Pili, utafiti huu unanuia kuwasilisha majanga ya kimazingira kama maudhui mengine katika fasihi kama vile: umaskini, ubaguzi wa jinsia, elimu na siasa. Huku ukitathimini nafasi ambayo mazingira huchukuwa. Mazingira yana sauti ambayo huwasilishwa kupitia majanga yanayosababishwa na ukosefu wa utunzaji wa mazingira (Couldry, 2010) na ni lazima waandishi waiwasilishe sauti hiyo kupitia kwa maandishi maandishi. Hivyo tunanuia kuonyesha jinsi mwandishi wa riwaya ya *Tikitimaji* (2013) na *Msimu Wa Vipepeo* (2006) anavyowasilisha masuala ya mazingira.

Utafiti huu pia unalenga kuwahamasisha waandishi wa fasihi wajikite zaidi kulenga masuala ya kimazingira ambayo ndicho kitovu cha uhai wa mwanadamu. Fasihi huweza kutumika kama nyenzo ya kuwahamasisha wanajamii kutenda jambo. Utafiti huu unakusudia kutathimini iwapo riwaya hizi mbili: *Tikitimaji (*2013) na *Msimu Wa Vipepeo* (2007) zinatosheleza majukumu haya katika jamii kwa kuwahamasisha kuhusu mazingira.

**1.6 Upeo na mipaka**

Kuna tanzu nne za fasihi andishi nazo ni: riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi andishi. Utafiti huu unazingatia utanzu wa riwaya pekee yake. Tanzu hizi nyingine zilifaa katika utafiti huu kubaini jinsi suala la mazingira lilivyoshughulikiwa katika tafiti za awali za tanzu hizo. Mwandishi amepata kuandika riwaya kumi; idadi ambayo inatokana na maelezo ya tovuti ya maktaba ya Chuo Kikuu cha Nairobi (2002-2015) kuhusu Wamitila, hata hivyo, riwaya za *Tikitimaji* na *Msimu Wa Vipepeo* ndizo zilizoteuliwa kimakusudi kwa sababu zilishughulikia maudhui ya mazingira moja kwa moja na zimeandikwa wakati maalum

Upeo wa utafiti huu katika riwaya hii unashughulikia uchanganuzi wa wahusika na jinsi mwandishi alivyowasawiri ili kudhihirisha na kupambanua maudhui ya mazingira. Ingawa katika riwaya hizi mwandishi alitumia wahusika wengi kuwasilisha ujumbe wake, utafiti huu unashughulikia tu wahusika ambao walisawiriwa kudokeza dhana za kimazingira. Matumizi ya lugha ni kipengele kingine cha fasihi ambacho utafiti huu ulishughulikia. Mwandishi wa riwaya hizi ametumia tamathali nyingi za usemi katika kuwasilisha ujumbe wake. Tuliangalia tamathali kama vile: takriri, tashbihi, istiari, taswira, methali, chuku na nahau. Hata hivyo utafiti ulichambua tu tamathali za lugha ambazo zilidokeza maudhui ya mazingira.

Katika kipengele cha maudhui, utafiti huu unashughulikia maudhui ya mazingira kama vile yalivyoshughulikiwa na mwandishi Wamitila katika riwaya zake mbili tulizoziteua. Kwa kutumia madhumuni ya tatu, tunatathmini msimamo wa mwandishi kuhusiana na suala la mazingira. Utafiti uliangalia jinsi msimamo wa mwandishi kuhusu suala hili la mazingira ulivyoakisi uhalisia wa maisha ya binadamu. Pia utafiti ulitathmini iwapo mwandishi alifaulu kuwasilisha maudhui haya ya mazingira.

Kwenye nyaraka za kimaandishi, utafiti huu ulishughulikia makala yaliyoandikwa kuhusu mazingira. Ripoti mbalimbali zinazoshughulikia mazingira, za kitaifa pamoja na za kimataifa zilishughulikiwa katika sehemu ya usuli. Hii ni kwa madhumuni ya kuchambua suala la mazingira kihistoria na kujua maendeleo ya maudhui haya ili tuweze kutathimini jinsi mwandishi Wamitila alivyowasilisha maudhui haya katika riwaya hizi mbili teule.

Utafiti huu ulizingatia ukusanyaji, uchanganuzi, ufasiri na uwasilishaji wa data ili kuelewa sifa mbalimbali za fasihi. Orodha ya uchunzaji ndicho kifaa kilichoteuliwa kukusanyia data. Data ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo kisha data iliwasilishwa kwa njia ya maelezo.

## 1.7 Hitimisho

Sura hii ilishughulikia hatua muhimu na za kimsingi za utafiti. Hatua hizi ni pamoja na: usuli wa utafiti, suala la utafiti,nadharia tete, malengo ya utafiti, sababu zilizopelekea utafiti huu kufanywa, mipaka ya utafiti na mwisho ni ufafanuzi wa istilahi kama zilivyotumika katika utafiti huu.

## 1.7 UFAFANUZI WA ISTILAHI

**Maudhui**- jumla ya mawazo yote yanayozungumzwa pamoja na mtazamo wa mwandishi juu ya mawazo hayo.

**Ekolojia** – Ni taaluma iyangaziayo mahusiano kati ya mazingira na binadamu.

**Fasihi mazingira**-ni nadharia inayoelezea uhusiano wa fasihi na mazingira.

**Ufeminsti wa kiekolijia**- ni mkabala uonyeshayo mahusiano kati ya mazingira na mwanamke.

## SURA YA PILI

## MISINGI YA KINADHARIA

### 2.0 Utangulizi

Sehemu hii ilifafanua yaliyoandikwa kuhusu mada, sehemu ambayo imefafanuliwa kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti. Pia nadharia zilizoongoza utafiti huu zilifafanuliwa. Utafiti ulitumia kiunzi cha nadharia kutoka kwa nadharia mbili ambazo ni uhalisia na nadharia ya fasihi mazingira. Mihimili faafu kwenye nadharia hizi mbili zilitumika.

### 2.1 Yaliyoandikwa kuhusu mada

#### 2.1.1 Fasihi mazingira

Baek, Cho na Koo (2008) katika makala yao ya *The environmental consequences of globalization: Acountry- Specific Time Series Analysis,* wanamnukuu Dean (2002) aliyesema kuwa uwazi wa kibiashara wa kimataifa umechangia pakubwa uharibifu wa mazingira. Sheria zilizowekwa ni legevu na haziwezi kudhibiti wafanyibiashara ambao azma yao ni kupata faida tu. Makala haya yanazungumzia nafasi ya utandawazi katika uharibifu wa mazingira. Utafiti huu uliangalia jinsi utandawazi huchangia uharibifu wa mazingira, pia ulinuia kuonyesha njia mwafaka za kukabiliana na utandawazi ili kuhifadhi mazingira. Makala haya yalifaa katika utafiti huu kuangalia jinsi wahusika mbalimbali walivyochangia uharibifu wa mazingira kiuchumi.

Utafiti uliofanywa na Arege katika mkusanyiko wa kazi za Slovic (2009), unasema kuwa waandishi wa Kiswahili kama vile Wa Mberia (2001*)* katika mkusanyiko wake wa mashairi ya *Bara Jingine* haswa katika mashairi ya: *Jinamizi, Nieleze, Ngoi na waimbaji, Ngao na Thagicu, Mimi mto Nairobi, Okidi apiga Ukelele na Bwawa la Ithanje*, anazungumzia suala la uchafuzi wa mazingira. Pia mashairi ya Kezilahabi (1974) katika diwani ya *Kichomi* kwenye shairi mahususi la *Uvuaji samaki Victoria.* Shairi hili linaelezea athari ya kuvua samaki kupita kiwango kinachostahili. Said

Ahmed pia amejifunga kibwebwe katika uandishi huu wa kiekolojia katika mashairi yake ya *Wawapi*, shairi ambalo linazungumzia kupotea kwa ndege asilia. Utafiti huu ulinuia kubainisha iwapo mwandishi Wamitila katika riwaya zake hizi mbili; Tikitimaji na Msimu Wa Vipepeo alishughulikia ipasavyo masuala ya mazingira. Je riwaya zake zitaweza kuitwa za kimazingira? Je ni mwandishi wa fasihi ambaye anaoanisha fasihi na mazingira? Hizi ndizo mianya ambazo utafiti huu ulinuia kuziba. Pia tulinuia kuonyesha jinsi mwandishi huyu ameonyesha masuala mbalimbali ya mazingira kama vile uhusiano wa binadamu na mazingira athari ya matendo ya binadamu kwa ekolojia na uwezo wa ekolojia kustahimili matendo haya kupitia kwa riwaya hizi mbili teule za Wamitila.

Adams na Slovic (2009) katika makala yao ya *The shoulders we stand on ecocriticism: An introduction to ethnicity*, wanachambua zaidi upangaji wa fasihi mazingira katika mikondo miwili, wa kwanza na wa pili. Wanasema kuwa mkondo mpya na ambao ni watatu, ni wa kutambua maadili na uhusika wa taifa huku ikipita mipaka ya kikabila na ya kitaifa. Mkondo huu unaangalia sura zote za uzoevu wa binadamu. Nia yao ni kuangazia majanga ya kimazingira na jinsi yanavyoathiri watu maskini na watu wa rangi tofauti tofauti. Utafiti huu ndio msingi wa fasihi mazingira na jinsi inavyojihusisha na masuala ya kijamii na kisiasa katika nchi za kimagharibi. Utafiti huu ulitusaidia kubainisha tabia ya wahusika katika kuchangia uchafuzi wa mazingira katika riwaya teule za Wamitila. Vilevile, uliangalia maudhui ya mazingira kama yanavyowasilishwa katika riwaya mahususi za Wamitila, *Tikitimaji* (2013) na *Msimu Wa Vipepeo* (2007). Nwagbara (2010), katika utafiti wake kuhusu uharibifu wa mazingira nchini Nigeria, anaeleza kuwa waandishi nchini Nigeria walitumia fasihi kuhamasisha jamii kuhusu uharibifu wa mazingira na athari yake kwa maisha ya binadamu. Nwagbara anaangazia mashairi ya Ojaide ya *Delta Blues and Home Songs*

*(1998)* na *Daydreams of Ants and Other Poems (1997)* ambayo madhumuni yake ni kuelezea uharibifu uliofanyiwa mazingira katika eneo la Delta nchini Nigeria. Hata hivyo utafiti huu uliangalia riwaya ya *Tikitimaji.* Utafiti huu ulinuia kutathimini iwapo riwaya hizi teule zinaweza kuhamasisha umma kuhusu majanga ya kimazingira. Kwa kawaida riwaya huwa utungo mrefu ambao husimulia matukio kwa kina. Iwapo tungo za shairi ziliweza kutumiwa kuwasilisha masuala haya ya mazingira basi riwaya huwa na nafasi ipi?

Kavila (2013) katika mada yake ya “The theme of environmental conservation in *Different Colours* and the *Terrorists of Aberdare* by Ng’anga Mbugua, anabainisha uhusiano wa uchafuzi wa mazingira na uhifadhi katika mazingira ya kiuchumi na kisiasa nchini Kenya. Utafiti huu haukushughulikia mifumo ya kijamii na michango yao katika uchafuzi wa mazingira mwanya ambao utafiti wetu unaziba. Utafiti huu uliangalia masuala ya mazingira, kuanzia kwa uasilia wa ulimwengu asilia na maliasili hadi kwa uchafuzi na juhudi za kuhifadhi.

Sangili (2014), katika makala ya *literary environmentalism*: *An ecocritique of Kiswahili literature* anashughulikia vitabu na mashairi yafuatayo: Riwaya ya *Nakuruto* (2009) iliyoandikwa na Momanyi. Riwaya hii inaangazia suala ya ufeministi wa kiekolojia. Mwandishi anamtumia mhusika Nakuruto kuhamasisha jamii kuhusiana na uharibifu wa mazingira. Katika hali ya kukomboa mazingira, mhusika Nakuruto anapitia changamoto nyingi sana haswa kwenye jamii yenye mifumo ya,, kiubabe-dume. Sangili (kt) anasema kuwa mhusika Nakuruto katika riwaya hii anasukumwa na sheria ya UNFCC (2009) ya uwajibikaji wa pamoja. Sheria hizi za UNFCC msingi wake unatokana na utafiti wa kisayansi ambao haukuhusisha asasi za kitamaduni. Mwandishi anakubaliana na Moore (2008) kuwa upo uhusiano wa moja kwa moja kati ya mazingira na mwanamke. Hata hivyo, utafiti huu ulishughulikia masuala ya mazingira

na uhusiano wao na mwanamke. Utafiti huu pia ulitathmini nafasi ya jinsia zote katika masuala ya mazingira na majukumu ya kila jinsia.

Riwaya ya pili anayoichambua sangili (2014) katika makala yake ni riwaya ya Mohamed, *Babu Alipofufuka* (2001). Ni riwaya inayoonyesha athari ya uharibifu wa mazingira. Mwandishi anatumia lugha rahisi na yenye mvuto kuelezea athari ya miale ya jua kwenye utosi wa binadamu. Ingawa wataalamu wa kisayansi wanaelezea kuhusu ongezeko la joto na hata kutupa idadi kamili kwenye vipimo, fasihi inatumia tu lugha ya maelezo kuwasilisha suala hili. Riwaya ya *Bustani ya Edeni* ni riwaya ya tatu aliyoshughulikia na pia kuangazia masuala ya mazingira. Ni riwaya inayoonyesha mazingira ya jana, leo na baadaye yalivyoghasiwa na tamaa ya binadamu, uchafu unajikunjua na usafi unajikunja, maji hayanyweki na hewa haivutiki hii yote ni kutokana na pupa ya maendeleo. Utafiti wa Sangili ulitufaa katika kubainisha matendo ya binadamu katika kusababisha majanga ya kimazingira. Hata hivyo utafiti huu haujaangalia riwaya ya *Tikitimaji* kama riwaya ya kimazingira. Basi utafiti huu ulijaza pengo hilo katika kuangazia riwaya hiyo ikiwa inatosha kuwa riwaya ya kimazingira.

Utafiti wa Sabula (2014), katika mada yake ya *Nafasi ya mwanamke katika uhifadhi wa mazingira: Mtazamo wa fasihi ekolojia kifeministi,* anaangalia namna mwanamke anahusika katika uhifadhi wa mazingira katika himaya zilizotawaliwa na ubabe-dume. Utafiti wetu unaangalia jinsia zote na matendo yao kuhusiana na ulimwengu asilia. Utafiti huu uliangalia jinsi mwandishi alisawiri wahusika wa jinsia zote katika katika kuwasilisha masuala ya mazingira.

Carol (2016), katika mada yake "Towards an African-Focused ecocriticism: The case of Nigeria", anachambua riwaya za Kinigeria zifuatazo: *Things Fall Apart* (1958) yake Achebe, *TheFamised Road* (1991) yake Okri, *Burning Grass* (1962) yake Kwensi, *The Voice* (1964) yake Okara, *Sozaboy* (1985) yake Saro- Wiwa na *Oil On Water* (2010)

yake Habila. Katika Makala haya, Carol anabainisha majanga ya kimazingira yanayosababishwa na ufukuzi wa maliasili na Wachina kwa hadaa za maendeleo na utandawazi. Utafiti wetu unaangalia riwaya za Wamitila na jinsi alivyowasilisha masuala ya mazingira kwa jumla, iwapo alifaulu kuwasilisha majanga ya kimazingira na njia maafaka za kukabiliana na majanga hayo bila kuhusisha utafiti wa kisayansi bali kupitia usanii wa lugha.

Mugwe (2018), katika mada, “Athari za mtaguzano kati ya jamii na ekolojia katika ushairi wa Kithaka Wa Mberia: *Bara Jingine na Rangi Ya Anga”*anajadili athari za masuala ya kijamii kwenye mfumo wa ekolojia kupitia uwasilishaji wa maudhui. Alibainisha maudhui katika mashairi haya mawili. Diwani hizi mbili zinasheheni mandhari na maudhui ambayo yanayonyesha jinsi mfumo wa ekolojia jamii ulivyoathiriwa na shughuli za wanajamii. Utafiti huu ulitusaidia kubainisha visababishi vya uchafuzi wa mazingira. Hata hivyo utafiti wetu ulikuwa tofauti kwa sababu uliangazia jinsi masuala ya mazingira yalivyowasilishwa kwenye riwaya teule za Wamitila.

### 2.1.2 Matumizi ya mtindo katika kuwasilisha maudhui

Kitsao (1975) katika tasnifu yake ya uzamili alishughulikia *Stylistic approach for the study of written swahili prose texts*. Alifafanua jinsi dhana ya mtindo hujitokeza katika kazi za kifasihi. Miongoni mwa kazi alizozishughulikia ni: *Rosa Mstika* (1971) na *Wasifu Wa Siti Binti Saad* (1960). Alihakiki matumizi ya mtindo katika riwaya, tamthilia, ushairi na hadithi fupi. Utafiti wa Kitsao uliafiki utafiti huu katika kupeana mwelekeo mwafaka wa kuvihakiki vipengele vya mtindo katika riwaya za *Tikitimaji* na *Msimu Wa Vipepeo*.

Mbatiah (2001), anasema kuwa tamathali za usemi ni ukiushi wa kimakusudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya maana na mpangilio wa maneno, ili kuleta

maana mpya au msisitizo. Naye senkoro (1982) anasema kuwa tamathali za usemi ni maneno, nahau, au sentensi ambazo hutumiwa na wanafasihi ili kutia nguvu maana, mtindo na hata sauti katika maandishi au usemaji. Kwa mujibu wa waandishi hawa wawili, tamathali za usemi husisitiza maana na ndiposa maoni ya waandishi hawa yaliafiki utafiti huu kueleza namna mwandishi alitumia tamathali za usemi kama mbinu ya kimtindo kusisitiza masuala ya mazingira katika riwaya teule za Wamitila.

Mohamed (2006) anabainisha mitindo mbalimbali inayojitokeza katika riwaya ya *Siku Ya Watenzi Wote* katika makala "mitindo katika riwaya ya *Siku Ya Watenzi Wote."* Matumizi ya mtindo maarufu wa uwili unajitokeza katika kila kitu kinachotajwa. Matumizi ya mtindo huu wa uwili unaibua maudhui ya ushikamano na umoja katika riwaya hii. Utafiti huu uliangalia suala hili la mtindo lakini kwenye riwaya mbili za Wamitila: *Msimu Wa Vipepeo (2006)* na *Tikitimaji (2013)*. Pia utafiti huu ni tofauti kwa sababu uliangalia mitindo mbalimbali katika riwaya hizi mbili na jinsi mitindo hiyo ilivyoibua na kukuza maudhui na dhana za mazingira.

Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa baadhi ya sifa na viwango vya lugha ya kiisimu humsaidia mhakiki kuichambua kazi ya fasihi. Kwa mfano, moja kati ya sifa bia za lugha ni utata. Lugha huwa na uwezo wa kueleza jambo moja kwa njia nyingi. Utafiti wetu ulinuia kuangalia jinsi mwandishi Wamitila alivyotumia lugha kueleza dhana ya mazingira kwa njia nyingi zinazovuta makini ya msomaji.

Wanyonyi (2009) alihakiki riwaya ya *Nyuso Za Mwanamke* ya S. Ahmed Mohammed. Katika kazi yake alishughulikia matumizi ya lugha kama vile lugha ya kitamathali, tasfida, ishara za uwashiriaji na maswali balagha. Hata hivyo kazi yake alielekeza katika mtazamo wa saikolojia-changanuzi, utafiti huu uliangalia mbinu mahususi za lugha alizozitumia mwandishi kuwasilisha maudhui ya mazingira katika riwaya za

*Tikitimaji (2013)* na *Msimu Wa Kipepeo (2006)* huku utafiti ukiegemea nadharia za uhalisia na fasihi mazingira.

Kanyua (2013), katika mada yake ya uzamili ya "Mtindo unavyoendeleza maudhui katika tamthilia ya *Natala",* katika sura ya nne anaangalia jinsi mwandishi alivyotumia lugha kuwasilisha maudhui katika tamthilia hiyo. Utafiti uliangalia jinsi mwandishi alivyotumia mtindo katika kuwasilisha maudhui mahususi. Mtindo uliangaliwa katika mkabala wa masuala ya mazingira katika riwaya ya *Tikitimaji (2013)* na *Msimu Wa Vipepeo (2006).*

Muthoni (2014) katika mada yake ya uzamili ya *Uhakiki wa maudhui na mtindo katika riwayaya Tikitimaji*", anafafanua matumizi ya tamathali za usemi na jinsi zilivyokuza maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Tikitimaji*. Utafiti huu uliangalia suala hili la mtindo lakini si kwenye kuwasilisha maudhui yote bali ni matumizi ya mtindo katika kuwasilisha masuala mahususi ya mazingira. Pia kwenye utafiti wake tamathali zingine kama taswira na maswali balaga hazikujadiliwa mwanya ambao tulinuia kuziba.

### 2.1.3 Matumizi ya wahusika katika kuwasilisha maudhui

Maudhui ni kile kisemwacho katika kazi ya fasihi. Ni jumla ya mawazo yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi ikiwa pamoja na falsafa na mtazamo wa mwandishi kuhusiana na mawazo hayo. Hujumuisha mawazo na mafunzo yanayomsukuma msanii kutunga kazi fulani ya kisanaa (Ntarangwi, 2004). Muindi (1990) aliainisha wahusika makahaba katika vitabu vya Said A Mohamed. Wahusika hawa wamepewa wasifu kimaumbile unaooana na majukumu waliYosawiriwa kutekeleza. Utafiti wetu kwa upande wake utaangalia wasifu wa wahusika kimaumbile na jinsi walivyotumiwa na mwandishi kusawiri maudhui ya mazingira.

Momanyi (2000) anaangalia suala la mhusika wa kike katika fasihi ya Kiswahili huku akibainisha tofauti iliyoko kati ya wahusika wa kiume na wa kike katika hali

mbalimbali. Utafiti wetu unaangalia usawiri wa wahusika wote kwa jumla katika fasihi na usawiri wao katika hali za kisiasa, kijamii na kiuchumi katika kuwasilisha maudhui ya mazingira. Otieno (2005) anazungumzia kuhusu matilaba na utendi wa malengo na wahusika kimsingi uumbaji wa wahusika na mahusiano yao wenyewe kwa wenyewe ni yale wanayoyaeleza na kuamini ni muhimu katika matilaba ya mwanadamu kwa kuwa humithilisha jamii halisi ya ulimwengu tunamoishi. Utendi wao (wahusika) katika kubainisha maudhui ya mazingira ni mwanya ambao tunanuia kuziba kwa kuonyesha jinsi matendo yao yanamithilisha ukweli wa maudhui ya mazingira katika utafiti huu.

Mulila (2005) aliandika kuhusu *muwala na mshikamano katika Kiswahili: Umuhimu wake katika uchanganuzi wa riwaya ya Vipuli Vya Figo*. Katika sura ya tatu aligusia usawiri na majukumu ya wahusika. Anasema kuwa udhibiti wa wahusika ni jambo ambalo huchangia mshikamano wa matini. Haitoshi riwaya kuwa na wahusika tu, wahusika hawa ambao ni mahususi katika riwaya fulani ni lazima watekeleze majukumu yao kisanaa katika riwaya hiyo. Utafiti wetu ulinuia kutathimini jinsi mwandishi alivyotumia wahusika kutekeleza jukumu la kuwasilisha majanga ya mazingira.

Murumba (2011) katika mada yake ya *mtindo katikaWatu wa Gehenna*" anashughulikia suala la uhusika na wahusika katika riwaya ya *Gehenna* katika sura ya pili. Anabainisha njia mbalimbali za kumsawiri mhusika zikiwemo: maelezo ya msimulizi au mwandishi, maelezo ya wahusika wengine, mbinu ya kidrama, mbinu ya majazi, mbinu ya ulinganuzi na mgotanisho na mbinu ya mwingiliano matini. Pia ameainisha aina ya wahusika katika makundi mawili, wakuu na wasaidizi. Utafiti huu wa Murumba unatuafiki katika utafiti wetu katika kueleza jinsi mwandishi wa riwaya ya *Tikitimaji (2013) na riwaya ya Msimu Wa Vipepeo (2006)* alivyowasawiri wahusika kuwasilisha maudhui ya mazingira.

Kisha, Rono (2013) alishughulikia uhakiki wa maudhui katika riwaya ya *Kidagaa Kimemuozea*. Katika sura ya tatu aliainisha wahusika kulingana na sifa zao. Tafiti hizi zote zilitusaidiakatika kubainisha wahusika katika riwaya teule pamoja na kupambanua majukumu yao haswa kwenye mkondo wa mazingira.

Wanjala (2015) katika mada ya *Usawiriwa malezi unavyoathiri utambulisho wa vijana katikariwaya ya Kiswahili* katika sura ya pili anashughulikia suala la uhusika wa vijana katika riwaya ya Kiswahili.  Anachambua matini teule ya: *FahariYa Mateso* (Oyoo, 2013), *Anasa* (Kingala, 1984 na *Asali Chungu* Said, A.M 1977). Anasema kuwa wahusika vijana katika matini hizi teule wametumiwa kuwasilisha ukweli wa malezi jinsi yanavyosawiri utambulisho wao. Utafiti unanuia kubainisha jinsi vijana kama wahusika wanavyosawiriwa na waandishi kuwasilisha maudhui teule katika jamii. Kwa mujibu huu maudhui ya masuala ya mazingira.

**2.2 Kiunzi cha nadharia**

Utafiti huu utatumia kiunzi cha nadharia kutoka kwa nadharia mbili: mihimili kutoka kwa nadharia ya uhalisia na nadharia ya fasihi mazingira. Nadharia ya uhalisia iliwekewa msingi na Hegel (1979), katika kitabu chake kilichojulikana kama *Introduction to Aesthetics*. Huyu anapendekeza matumizi ya neno “uhalisia” kuelezea kazi za kifasihi ambazo huwasilisha ulimwengu na maisha ya kijamii ambako kuna wahusika au mhusika anayetenda mambo kwa jinsi inayochochewa waziwazi na hali aliyomo. Nadharia hii iliasisiwa karne ya kumi na tisa na kufafanuliwa zaidi na Groffman (1952).

Kwa mujibu wa Ntarangwi (2004), anasema kuwa nadharia hii upana wake unamaanisha uwakilishi wa uhalisi wa mambo katika fasihi. Nadharia hii ilizuka katika karne ya kumi na tisa ili kupinga mkondo wa kiulimbwende. Mhakiki wa kihalisia anaamini katika matokeo ya mambo na ukweli na ukweli anaouzingatia ni ule ambao

unaweza kuonekana na kuthibitiwa na tajriba. Nadharia hii hupembenua namna mwandishi alivyodhihirisha uhalisia wa mambo kupitia maudhui aliyoyazingatia. Msanii anapaswa kusawiri wahusika, matukio na mandhari yanayokubalika na kuaminika katika jamii. Ufahamu wa mazingira na maisha anayoyalenga mtunzi ni nguzo muhimu kwa mhakiki wa kihalisia.

Kulingana na Msokile (1993), anasema kuwa uhalisia ulianza mwaka wa 1820. Msingi wake ukiwa kuwa Sanaa inafaradhiwa iseme ukweli, iwe aminifu na ionyeshe hali halisi ya mazingira. Nadharia hii inapendekeza ujenzi wa wahusika wanaolingana na hali halisi na maisha yaani awe mhusika wa sura ileile sawa ya maisha ya kawaida kwani sanaa inafaa kueleza ukweli na inafaa kueleweka.

Dhana ya uhalisia hutumika kuakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na mazingira. Kama asemavyo Wamitila (2007), uhalisia unahusishwa na kipindi maalum kihistoria katika jamii za Ulaya. Kipindi hiki kinahusishwa na waandishi kama vile Balzac, Stendhal na Flaubert. Waandishi hawa wanasisitiza maelezo ya kikweli katika kazi zao na waliamini kuwa dhima ya mwandishi ni kuonyesha ukweli jinsi ulivyo. Fasihi yoyote lazima ionekane kama kioo cha jamii. Hivyo basi ni lazima jamii iweze kujitazama na kujiona kupitia fasihi.

Utafiti huu uliongozwana mihimili ifuatayo ya nadharia hii:

a) Kazi ya msanii inapaswa kuwasilisha ukweli kama ulivyo katika mazingira yake. Mhimili huu unatuonyesha jinsi maudhui ya mazingira yanavyojibainisha kihalisia.
b) Kazi ya fasihi inajitosheleza. Riwaya za Tikitimaji (2013*)* na *Msimu Wa Vipepeo* (2006) ni kazi za kisanaa kwa vile ina msuko, mtindo, wahusika na ujumbe.
c) Msanii anaangalia matatizo na kuchunguza chanzo chake. Anachunguza mabadiliko ambayo hutokea kwa kipindi cha kihistoria na kuyatumia kuyasawiri wahusika wake. Mhimili huu unatusaidia kubainisha vyanzo vya mabadiliko ya

mazingira kihistoria pamoja na mabadiliko ya wahusika katika vipindi mbalimbali vya kihistoria kwa mujibu wa ploti ya riwaya.

d) Wahusika ni vielelezo yakini vya binadamu wa kawaida kwa vile wao hutumia lugha ya kawaida kumwezesha mwanadamu kujifafanulia uwezo wake wa kutenda mambo na mtazamo wake kuhusu maisha. Mhimili huu unatusaidiakuonyesha kuwa wahusika kwenye riwaya hizi wanaathiriwa na yale wanayoyapitia.

**Nadharia ya fasihi mazingira**

Fasihi mazingira ni nadharia ambayo ina matapo katika fasihi ekolojia Kiafrika, Kimarekani na kifeministi huku ikihusisha mikabala mingine ya uhakiki katika fasihi ya Kiswahili kama vile ufeministi, umaksi na mkabala wa kibaada ukoloni. Nadharia hii inaangalia uhusiano wa fasihi na mazingira asilia. Barry (1995) anasema kuwa neno fasihi mazingira uasilia wake umehusishwa na Ruckert (1978) katika makala yake ya " *literatureand ecology, an experiment in ecocriticism*, ambayo iliendelea kukuwa hadi miaka ya 1989 katika mkutano wake wa fasihi mazingira (*world literature association*) huko Cour d'Alene ambapo Glotfelty (1996) alipochanganua upya neno hili na kueleza kuwa ni usomaji wa waandishi wa mazingira, dhana ambayo iliungwa mkono katika mkutano wa "*Western Literature Association* na Glen Love, na kufafanua kuwa fasihi mazingira ni uhusiano wa fasihi na mazingira. Anasema kuwa usomaji huu huchukuwa mtazamo wa kiardhi kama ilivyo tu ufeministi ambao huchukuwa mtazamo wa kijinsia na umaksi ambao huchukuwa mtazamo wa kimatabaka na uchumi. Fasihi mazingira hujihusisha na matendo ya binadamu, uhusiano wa binadamu na vitu vilivyo na uhai na visivyo na uhai. Pia nadharia ii hii huangalia uchangamano wa uhusiano kati ya maliasili na utamaduni. Rigby (2007) anaeleza kuwa nadharia hii ya fasihi ya ekolojia imejitokeza kubadili hali halisi ya uharibifu wa ekolojia kwa kuchanganua uamilifu wa kimaudhui, kisanii, kijamii, kihistoria, kiitikadi na kimbinu katika ekolojia asilia au

vipengele vyake kama vinavyohusishwa katika fasihi. Nadharia hii ilitokea katika mikondo miwili, wa kwanza na wa pili. Mkondo wa kwanza ulitokea miaka ya themanini kuelekea miaka ya tisini. Vigogo wa mtazamo huu wanadai kwamba uandishi wa fasihi ulenge ekolojia na dhana za ekolojia. Unaangalia majanga za ekolojia katika karne hii huku ikibaini kuwa sayansi imejihusisha sana na masuala ya mazingira kwa hivyo wakati umewadia wa fasihi kujihusisha kikamilifu na masuala haya kwani fasihi huingiliana sana na utamaduni wa maisha ya binadamu. Katika mkondo wa pili, Garrard (2004) anaangalia mipaka iliyoko ya ubinadamu na uso ubinadamu. Pia alifasiri upya neno mazingira kumaanisha maliasili. Kama asemavyo Beull (1995), ni kutokana na ufasiri ndipo palipoibuka makongamano kuhusu haki ya mazingira asilia. Kwa mujibu wa Glotfelty na fromm (1996), Greenblatt (1992), Beull (1995): nadharia hii huangalia mielekeo ya binadamu kuhusu mazingira, huangalia matumizi ya dhana za ekolojia katika kazi za kifasihi, hujihusisha na nguvu za kibinadamu na lugha ya binadamu kuhusiana na mazingira, huangalia mitindo ya lugha na jinsi mitindo hiyo huathiri namna binadamu anavyotagusana na mazingira, nadharia hii huchukulia kwamba mazingira na utamaduni hushirikiana katika ujenzi wa lugha na fasihi, binadamu hawezi kuishi bila ekolojia lakini ekolojia huweza kuishi bila binadamu, huangalia jinsi waandishi huwakilisha masuala ya mazingira na jinsi kazi hiyo huathiri mielekeo ya ulimwengu katika hali halisi na mwisho huangalia uwezo wa lugha katika kuwasilisha masuala ya mazingira. Nadharia hizi mbili zinachangia katika kuthibitisha nadharia tete za utafiti huu. Nadharia ya fasihi mazingira imetumiwa kuchanganua na kubainisha dhana za ekolojia kama vile viwango vya mpangilio wa kibiolojia, viumbe asilia, uwezekano wa ekolojia kustahamili matendo ya uchafuzi na kurejelea hali asilia pamoja na mitindo ya lugha iiliyotumika kuwasilishia dhana hizi za

ekolojia. Huku nadharia ya uhalisia ikinisaidia ikitumiwa kubainisha ukweli wa masuala ya mazingira katika kazi za fasihi.

## 2.3 Hitimisho

Sura hii iliangazia kiunzi cha nadharia na mapitio ya maandishi kwa mujibu wa yalioandikwa kuhusu mazingira, maudhui na mitindo ya lugha katika kuwasilisha maudhui sawa na wahusika. Katika mapitio ya fasihi mazingira, mwanya ambao utafiti uliziba ni nafasi ya wahusika wote, waume kwa wake katika utunzaji wa mazingira. Upo uhusiano wa karibu sana kati ya mazingira na mwanamke. Je jinsia zote zaweza kuwa na nafasi iyo hiyo ya kutunza mazingira? Kuhusu mtindo na uwasilishaji wa maudhui, utafiti wetu ulionyesha S jinsi uteuzi wa mbinu mwafaka unafaulisha uwasilishaji wa maudhui mahususi ya masuala ya mazingira. Tafiti nyingi sana zimeandikwa kuhusu matumizi ya mitindo katika kuwasilisha maudhui. Utafiti wetu ni tofauti kwa kuwasilisha uhusiano uliopo kati ya mitindo ya lugha na ukuzaji wa maudhui ya mazingira katika riwaya teule za Wamitila: *Msimu Wa Vipepeo* (2006) na *Tikitimaji* (2013)

# SURA YA TATU

# NJIA NA MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Sehemu hii ilielezea muundo wa utafiti, kundi lengwa, usampulishaji, ukusanyaji data, uchanganuzi wa data, uhalali na kuaminika kwa vifaa vya kukusanyia data, maadili ya utafiti pamoja na uwasilishaji wa data hiyo.

## 3.1 Muundo wa utafiti

Muundo wa kiuchanganuzi ni mpangilio ambao mtafiti hutumia data ambayo iko tayari kisha huichanganua kulingana na mada ya utafiti husika. Mbinu hii iliafiki katika utafiti huu kwa sababu data ambayo ilitafitiwa ilikuwa tayari na iliichanganua kwa mujibu wa mada ya utafiti. Riwaya teule za Wamitila tayari zimekwisha andikwa na ilichanganuliwa kuona nafasi ambayo fasihi huchukua katika kuwasilisha masuala ya mazingira ili kuthibitisha nadharia tete. Muundo wa utafiti kwa mujibu wa Kothari (2008), hutoa taswira kamili inayoonyesha namna utafiti ulivyofanyika tangu mwanzoni hadi tamati. Utafiti huu ulitumia muundo wa kiuchanganuzi.

## 3.2 Eneo la utafiti

Eneo kithematiki ni vitabu vya Wamitila vya *Tikitimaji* (2013) na *Msimu Wa Vipepeo* (2006). Utafiti huu ulishughulikiwa kulingana na jinsi mwandishi alivyowasilisha maudhui ya mazingira katika riwaya hizi teule.

## 3.3 Kundi lengwa

Kwa mujibu wa Cresswell (2009) anaeleza kundi lengwa kuwa wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au elementi ambazo mtafiti alikusudia kutumia katika utafiti wake. Kundi lengwa katika utafiti huu ni riwaya za Wamitila. Wamitila (1999), katika makala ya *"Place and placelessness* in *Kiswahili literature: The role of setting in Kiswahili creative writing*" anaangalia nafasi ya mandhari katika riwaya, ambapo anasema kuwa

inapaswa mtu kusoma mazingira katika mandhari ya matini husika. Kwake mandhari huweza kutumika kuelezea hali ya mazingira ijayo. Tuliteua vitabu vya Wamitila kwa sababu kutokana na makala haya anaonyesha ari katika uwanja huu wa fasihi mazingira. Pia tulitaka kutathmini iwapo uandishi wake haswa riwaya zake za hivi karibuni zilivyoshughilikia masuala haya ya mazingira kupitia mitindo na wahusika ambapo mitindo ni sehemu ya mandhari.

### 3.4 Usampulishaji

Riwaya za *Tikitimaji (2013)* na *Msimu Wa Vipepeo (2006)* ndizo matini zilizochaguliwa kimakusudi na mtafiti. Mtafiti alifikia sampuli hii baada ya kusoma riwaya za Wamitila na kuteua kimakusudi riwaya hizi kwa sababu riwaya hizi zinazungumzia masuala ya mazingira. Uteuzi wa kimakusudi huhusisha kuteua data kutoka kwa watafitiwa kulingana na sifa ambazo wanazihodhi. Mtafiti huamua kuteua ujumbe ambao anataka ujulikane kwa watu na huamua kwenda nyanyani kwa madhumuni ya kuwatafuta watu hawa ambao hujitolea kulingana na maarifa au uzoefu wa mada ambayo mtafiti ameiteua (Benard 2002). Data ilipatikana kutoka kwa matini hizi kimakusudi yaani kubainisha maudhui hayo kutokana na wahusika na pia mitindo na kuyahusisha na uhalisia ikitathimini kufaulu kwa mwandishi.

### 3.5 Ukusanyaji Data

Njia kuu ya kukusanya data ilikuwa uchunzaji ambapo mtafiti alitumia orodha ya uchunzaji kama kifaa cha kukusanyia data. Mtafiti alinukuu sehemu zenye kuashiria maudhui ya mazingira. Pia aliorodhesha wahusika na mitindo uliotumiwa kuwasilisha maudhui ya mazingira. Mtafiti atahusisha mbinu ya usomaji makini ili aweze kuthibitisha nadharia tete yake. Kwa mantiki hii, mtafiti alisoma riwaya za *Tikitimaji (*2013) na *Msimu Wa Vipepeo* (2006) kwa kuangalia vipengele husika vya utafiti wake.

**3.6 Uchanganuzi wa data.**

Utafiti huu ulichambua data kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo. Uchanganuzi wa yaliyomo kwa mujibu wa Yang (2008) huhusisha uchambuzi wa kiutaratibu wa matini iliyoteuliwa. Naye Krippendorff (2004), anasema huwa mbinu huu huhusisha matumizi ya ujumbe rudilifu na ambayo ni halali katika kuyahusisha masuala ya matini kwa masuala mengine yaliyo nje ya matini. Utafiti huu ulitumia mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo mbinu ambayo hutathimini uzito wa kutokea kwa neno au wazo katika utafiti. Uchanganuzi huu huelezea kimfumo yaliyomo katika data ya mwandishi au maongezi. Katika kufasiri yaliyomo uzito wa kutokea kwa jambo huwa ndio kipimo cha umuhimu au msisitizo. Fasiri za jambo hilo ni lazima ijikite katika madhumuni ya utafiti. Mbinu hii (ya uchanganuzi wa kiyaliyomo) iliwezesha mtafiti kuchunguza nafasi iliyopewa masuala ya mazingira katika riwaya hizi mbili teule.

**3.7 Uhalali wa data.**

Uhalali wa utafiti huu ulitokana na ukweli kuwa vitabu hivi vya Wamitila (riwaya ya *Tikitimaji na Msimu Wa Vipepeo*) vipo na vimeandikwa na pia vinapatikana katika maeneo ya kuuzia vitabu. Kila mwanajamii anaweza kuvipata na kuvisoma.

**3.8 Kuaminika kwa kifaa cha kukusanyia data**

Kuaminika kwa data za utafiti kulitokana na uwezo wa mbinu za utafiti kuwasilisha matokeo yale yale pale pale utafiti utakaporudiwa kwa kutumia mbinu zilizile (Kothari, 2008). Mbinu iliyotumiwa kukusanya data na data iliyokusanywa tayari imekwisha andikwa. Imetumika katika tafiti nyinginezo na kufaulu kutoa data ya kuaminika. Kifaa hiki cha orodha ya uchunzaji kitakuwa na mwongozo wa mbinu na wahusika tutakaotumia katika uchambuzi wa matini, utafiti uliangalia data ambayo tayari imekwisha andikwa na kunukuu aina ya mitindo ya lugha kama inavyowasilisha

maudui ya mazingira pamoja na kuangalia mbinu zilizotumiwa kusawiri wahusika kwa mujibu wa kifaa cha utafiti

### 3.9 Uwasilishaji wa matokeo ya utafiti

Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Maelezo hayo yanahusu jinsi maudhui ya mazingira yalivyosawiriwa katika riwaya ya *Tikitimaji* na *Msimu Wa Vipepeo*. Kwa njia ya maelezo, mtafiti aliorodhesha mbinu za lugha zilizotumiwa na mwandishi kudokeza maudhui ya mazingira. Pia mtafiti alishughulikia wahusika jinsi walivyosawiriwa na mwandishi ili kukuza maudhui haya ya mazingira. Mifano ilinukuliwa ili kuelezea mbinu alizozitumia mwandishi kubainisha maudhui ya mazingira kwa mujibu wa malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia mbili zilizoteuliwa.

### 3.9.1 Maadili ya utafiti

Jambo la muhimu lililozingatiwa katika utafiti huu ni kupata kibali cha cha utafiti kutoka kwa idara ya NACOSTI, kabla ya kwenda nyanjani. Utafiti huu ulizingatia haki za mwandishi wa riwaya ya *Tikitimaji na Msimu Wa Vipepeo*, ulishughulikia maudhui, mitindo ya lugha pamoja na wahusika jinsi yalivyowasilishwa na mwandishi riwayani bila kuongezea au kupunguza mada. Aidha, maisha binafsi ya mwandishi hayakuhusishwa kwenye utafiti huu.

### 3.9.2 Hitimisho

Sura hii iliangazia: muundo wa utafiti ambao utafiti uliteua muundo wa kiuchanganuzi, eneo la utafiti, usampulishaji ambapo mbinu ya uteuzi wa kimakusudi ilijadiliwa kama mbinu mwafaka. Kundi lengwa, ukusanyaji data, uchanganuzi wa data, uhalali, maadili na kuaminika kwa data na matokeo na uwasilishaji wa data pia ni mambo muhimu ambayo yalijadiliwa katika sura hii.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI WA WAHUSIKA NA LUGHA KITAMATHALI NA JINSI ILIVYOKUZA MAUDHUI YA MAZINGIRA

## 4.0 Utangulizi

Katika sura hii niliangazia dhana ya uhusika na  sifa mojawapo ya lugha ya kifasihi ambayo ni tamathali za usemi. Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), tamathali za usemi ni semi fupifupi zilizojengwa kwa lengo la kuwasilisha dhamira kwa hadhira iliyokusudiwa na kwa namna ya kuifikirisha hadhira husika. Naye Wamitila (2003) anatoa mifano ya tamathali za usemi kama vile: tashbihi, tashihishi, balagha, sitiari, takriri, tasfida na taswira. Katika utafiti wetu tumeangazia zile mbinu ambazo mwandishi wa riwaya ya Tikitimaji (2013) na Msimu Wa Vipepeo (2006) alitumia ili kuendeleza masuala ya mazingira.

## 4.1 Usawiri Wa Wahusika Katika Kuwasilisha Maudhui Ya Mazingira

### 4.1.1 Dhana ya uhusika

Suala la uhusika katika katika fasihi limejadiliwa na waandishi mbalimbali. Kulingana na Baldiac (2007), neno wahusika linatokana na kazi ya Theophrates "the characters" akieleza dhana ya mhusika. Wahusika huwa watu, wanyama au vitu katika kazi ya fasihi (Msokile,1992).  Dhana mbalimbali katika fasihi huwakilishwa na wahusika walioteuliwa na mwandishi. Sifa pambanuzi ambazo wahusika hawa huhodhi ndizo mwandishi wa kazi ya fasihi hutumia kuwasawiri kwa msomaji wake.

Wahusika hawa hutumia lugha na mitindo ya lugha katika kutagusana kwao ili kujenga tabia na hali za kisanaa. Mwandishi wa kazi ya fasihi huteua wahusika na kuwapa kazi zinazotofautiana miongoni mwao. Utofauti huu hutegemea lengo lake la uandishi. Sababu nyingine inayoleta utofauti huu ni aina ya sanaa ambayo mwandishi huteua na

ile ambayo inaweza kuathiri wahusika na jinsi watakavyosawiriwakuaminika kwao, wanavyohusiana wao kwa wao, uwakilishi wao na majina yao.

Wahusika ni nyenzo kuu katika fasihi kwa sababu wao ndiyo nguzo ya matendo yanayopatikana katika kazi ya kifasihi inayohusika (Wamitila, 2008). Mtazamo wa dhana ya uhusika hutegemea mkabala anaouchukua mhakiki na nadharia ya fasihi iliyotumiwa. Katika utafiti huu tutaangalia nadharia ya uhalisia na nadharia ya fasihi mazingira. Katika mkabala wa uhalisia tutaangalia namna mwandishi alivyowasawiri wahusika katika riwaya hizi mbili ili kuonyesha uhalisia wa masuala ya mazingira. Msingi mkuu wa fasihi ni ulimwengu halisi.

Uchunguzi wowote wa wahusika lazima uzingatie uhusiano uliopo kati ya wahusika na elementi nyingine katika kazi husika. kwa maoni ya Kundera (2007), wahusika wa kifasihi hawapaswi kupendwa kutokana na maadili yao bali ni kile wanachotakiwa kufanya ni kueleweka. Upo mwelekeo mkubwa wakuwachunguza wahusika kifasihi kwa kuwafungamanisha binadamu halisi na hata kutokana na mielekeo ya kimaadili au tabia, tukitarajia kuwa wahusika wale wakuu watakuwa na maadili fulani.

Wahusika husawiriwa kwa namna inayoingiliana na maudhui na hii hujitokeza kimaneno, kitabia na kimatendo. Wahusika ni sehamu ya fani na ni viumbe wa sanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira ya msanii. Mazingira haya yaweza kuwa ya kijiografia, kihistoria, kijamii, kitamaduni au kisiasa (Njogu & Chimera, 1999).

### 4.1.2 Uainishaji wa wahusika

Wahusika huainishwa kutegemea majukumu yao. Katika tasnifu hii, wahusika watainishwa kuzingatia njia mbili ambazo ni sifa zao na nafasi zao kuhusiana na masuala ya mazingira. Pia tutataelezea tu kwa ufupi njia nyingine za kuainisha wahusika. Wahusika wameainishwa kulingana na sifa zao kama ifuatavyo; wahusika wa miraba minne na wahusika wa mraba mmoja (Chimera na Njogu, 1999). Kwa

kuzingatia mawazo ya Forster (1927), Wamitila (2002) anainisha wahusika katika makundi mawili. Anainisha wahusika bapa na wahusika duara. Anasema kuwa wahusika duara mara nyingi hupatikana katika riwaya za kisiasa na hukaribiana kwa kiasi kikubwa na binadamu wa kawaida.

Uduara wa wahusika umo kwenye mabadiliko ya kitabia, kimawazo na kijamii na ndio huongoza hali halisi ya maisha ya mhusika. Wahusika bapa hutumiwa na mwandishi kusimamia dhana fulani. Wahusika hawa huwa hawabadiliki kutoka mwanzo wa hadithi hadi mwisho. Kuna aina mbili ya wahusika bapa nao ni wahusika sugu na wahusika vielelezo. Wahusika sugu hujulikana kulingana na maelezo ya msanii. Wahusika vielelezo hupewa majina kulingana na matendo na tabia zao.

Kunao wahusika ambao huchukuwa nafasi kuu katika kazi za kifasihi. Wamitila (2002), anasema kuwa kunao wahusika ambao husheheni hadithini kutoka mwanzo hadi mwisho na migogoro yote ya hadithi huwahusu. Pia kuna wale wengine ambao husaidia kukuza msuko wa hadithi na hawa huitwa wasaidizi. Sifa za wahusika hawa hubainika wanapoingiliana na wahusika wengine.

### 4.1.3 Njia nyingine za kusawiri wahusika

Kulingana na mpito wa wakati kihistoria, ndivyo wahusika wa kazi za fasihi wanavyozidi kubadilika. Mlacha na Madumulla (1991), wanasema kuwa wahusika wameainishwa katika makundi manne. Mhusika mkweza, mhusika wa kihalisi, mhusika wa kisiasa na mhusika wa kidhanaishi. Uainishaji huu umerejelewa na Njogu na Chimera (1999) katika makala ya *ufundishaji wa fasihi*. Wamitila (2002), naye anainisha wahusika katika makundi manne pia; mhusika wa jadi, wa kimuundo, kihalisi na wa kisasa.

Katika utafiti wetu, maelezo ya waandishi hawa yatatufaa sana. Tutakapokuwa tunabainisha njia mbalimbali alizotumia mhusika kusawiri wahusika ili kudhihirisha na

kukuza maudhui ya mazingira katika riwaya zake mbili teule. Ingawa wahusika wamesawiriwa kijamii, kitamaduni,

### 4.2 Wahusika katika riwaya ya Tikitimaji

#### 4.2.1 Zinji, Kombo, Maya na Sapna kama vielelezo wa uzinduzi wa mazingira.

Hawa ni wahusika wakuu katika riwaya hii. Wamelelewa katika makao ya watoto ya Quadulupe yaliyosimamiwa na Rehema. Ni kupitia safari yao kuelekea Tikitimaji ndipo mwandishi anafahamisha wasomaji kuhusu hali tofauti tofauti ya mazingira. Zinji anarejea alikozaliwa kuuliza ami yake kuhusu urithi wake.

Zinji ni mhusika kielelezo wa kuzindua jamii na kuihamasisha kuhusiana na suala la uchafuzi wa mazingira. Ni mtambuzi kwa sababu wanapofika Ganjoni, aliweza kubaini tofauti ya hewa ya pale. Anasema kuwa hewa ya pale ilikuwa yenye joto jingi na haikufanana na ile waliokuwa wameizoea. Kupitia jicho lake la utambuzi anabaini kuwa ingawa mama Rehema alikuwa amemweleza kuwa njia ya kuelekea Tikitimaji ilikuwa na miti mingi ajabu, anakagua njia ile na kusema kuwa miti haikuwa mingi na palikuwa na dalili za kukatwa kwa miti.

Yeye kama msimulizi wa hadithi anaendelea kukagua ile njia ya kuelekea Tikitimaji. Anasema kuwa njia ile ilikuwa imeingia kwenye mteremko ambapo mizizi ya miti iliyokuwa juu ilijitokeza kama matanzu ya mgunga mweupe. Kupitia maelezo yake msomaji anapata taswira kamili ya mmomonyoko wa udongo wa mazingira katika maeneo yale, ni kupitia kwa Zinji ndipo mwandishi anatuelezea kuhusu kupungua kwa maji katika mto Unasi kiasi kwamba sakafu yake ilionekana. Maelezo haya yanapatikana katika ukurasa wa 24. Mto huu uliathiriwa na matendo ya binadamu kwani sakafu ya mto huu ilifukuliwa kwa shughuli za kufukua mchanga kwa ujenzi.

Pia Zinji anatambua miale ya jua iliyokuwa inazidi kuongezeka kadiri walivyoendelea kukaribia Tikitimaji akilinganisha na mji wa Ganjoni walipokuwa wanataka. Uharibifu

wa hewa ulikuwa umeenea kote kote. Ukali huu wa miale ya jua unashadidia matendo ya binadamu ambayo yamepunguza utandu wa ozone na kuifanya kuachilia jua kali. Ni kupitia kwa Zinji ndipo tuanaelezwa kuwa habari kuhusu uharibifu wa mazingira zilipeperushwa kwenye vyombo vya habari lakini hali hiyo haikutiliwa maanani. Anasem kuwa kisa cha kuuzwa kwa mlima Trimacho kingekuwa kisa kizuri cha kuweka magazetini. Mhusika huyu ana ari ya kuwahamasisha wanajamii wote kupitia vyombo vya habari kuhusu kuonewa kwa mazingira.

Kupitia jicho lake la utambuzi, anatambua harufu kali kwenye lango kuu la Tikitimaji inayowashinda kupumua huku wakiwa wamefunga pua zao ili wasivute ile harufu. Anabainisha kuwa mwalimu Insafu alipenda kukaa sehemu yenye utulivu kwani kila sehemu ilijaa vumbi. Katika ukurasa wa 89, zinji anatueleza kuwa kando kando mwa barabara palirundikwa rundo la takataka.

Kombo ni polisi tofauti anayetafuta ukweli kuhusu Tikitimaji na kuleta haki kwa watu wote yakiwemo mazingira. Yeye ni jasiri na anawapa wenzake ulinzi wakiwa safarini. Katika ukurasa wa 47 Kombo anamdadisi mfugaji ifuatavyo:

> *"Kombo aliyekuwa mchokozi miongoni mwetu sote, akamuuliza kama hapakuwa na malisho huko alikotoka. Akasema kuwa hamna.*
>
> *"kwa nini malisho yamekuwa madogo?"*

Kupitia sifa yake ya udadisi, anabaini kuwa hapakuwa na malisho Tikitimaji. Kama anavyosema Reuvy (1999) kuwa mazingira yanapokuwa chafu binadamu huzoea hali ile. Ubinafsi umewasonga watu na hawatilii maanani matendo yao. Katika ukurasa wa 90, Kombo anatambua kuwa:

> "Tatizo *kuu la binadamu ni ubinafsi wa watu ambao hawachunguzi athari ya matendo yao"* (uk.90).

Mhusika mkuu wa tatu ni Sapna. Ni msichana aliyechanganya rangi, hali iliyompelekea kubaguliwa na kuishia kuwa mtoto wa jaa. Ni mtetezi wa mazingira. Anawahamasisha wanajamii kupinga uchafuzi wa mazingira kupitia kundi la WAZALIMA. Kundi hili liliongoza maandamano mjini na hata Tikitimaji. Katika ukurasa wa 26 Sapna anabaini kiini cha uharibifu wa mazingira. Anasema kuwa:

> *"Hata! Haya ya maji kukauka mtoni tunayasababisha wenyewe! Vitendo vyetu vinayasonga koo mazingira yenyewe! Na tukiendelea hivi kiwiliwili cha mazingira kitasakamwa hadi kitoke ngama," akatulia kabla ya kuendelea, "kumbukeni kisa cha kijijini tulikotoka. Zamani kulikuwa na miti iliyoifanya jiji ipendeze…kisha tukafanya nini? Miti tukaipukuta yote ili tuanze kuyapanda majengo. Ndege walioimba nyimbo za kupendeza wakanajiri. Wakabaki wakipongeza ujinga wetu.*

Katika ukurasa wa 87, Sapna anatambua uchafuzi wa hewa kwa kubaini harufu ya uozo wa hewa. Vitendo vya binadamu viliathiri mazingira. Kulingana na mhimili wa fasihi mazingira kuwa fasihi lazima iwasilishe mielekeo yetu kuhusu mazingira. Basi Sapna ana mwelekeo hasi kwa watu ambao wanayachafua mazingira. Kwa mujibu wa Sapna, mazingira yalikuwa yamechafuliwa kiasi kwamba pua za wengi zilifiliji na kukosa uwezo wao wa kimsingi. Katika ukurasa wa 89, anazindua umma kwa kuongoza usafi wa mji. Anawashawishi wakaazi pale waache kutupa taka karibu na lango kuu.

*Kumbe huku wanafanya yale yale makosa yetu? Akauliza Sapna. Baada ya muda akaendelea," sasa barabara nzuri kama hii itapakanaje na pande la mlima la uchafu kama hili!" …nilizikumbuka juhudi za Sapna na kundi lake za kuusafisha mji wa tulikotoka* (uk.89).

Nafasi anayoichukua mhusika huyu Sapna inaoana na nafasi ya mhusika Nakuruto katika utafiti wa Sabula (kt). Msukumo wa sapna unatokana na sheria za UFCC (2009)

za uwajibikaji wa pamoja. Kweye utafiti huu, jinsia zote zilihusishwa katika harakati za kukomboa mazingira.

Anawazindua wanajamii na kuwaeleza kuwa makosa wanayofanya mjini ya kurundika takataka kandokando mwa barabara si sura nzuri. Anashangazwa jinsi barabara nzuri kama ile ilivyopatikana na rundiko ya takataka. Katika ukurasa wa 90, kupitia usimulizi wake anasimulia kisa cha mchuuzi aliyeuza njugu zilizometameta ngozi. Anazichukua njugu hizi na kuzipeleka kwenye maabara ili zifanyiwe uchunguzi. Anagundua kuwa njugu zile zilikuwa na chembechembe za risasi. Ni kutokana na ubinafsi wa binadamu pamoja na tamaa ndipo hali yetu na ya mazingira huzorota. Piaanawaeleza wasomaji kuwa ipo hatari kubwa sana kwa maisha ya binadamu anapotumia vinywaji vilivyo na kemikali uk, 91.

Isitoshe, anatambua matatizo ya umwagaji ovyo wa taka kwenye mito mjini. Ni mkombozi wa mazingira. Katika uk, 125 anasema:

*"Nasema hivi: ukitaka kuyaharibu maisha ya binadamu, yaharibu mazingira yake… ukitaka kumuua binadamu, yaue mazingira yanayomhifadhi. Pana ufaano mkubwa baina ya mtu na mazingira; baina ya mtu na asili," akasema na kutua"* (uk.125).

Mwanadamu anaingiliana sana na mazingira asilia na anaeleza kuwa ukitaka kuyaharibu maisha ya binadamu haribu mazingira yake. Anasema kuwa mazingira yapo kwa ajili ya binadamu. Binadamu hapaswi kuwazia matakwa yake tu bali pia ya mazingira. Anasisitiza mhimili katika fasihi ekolojia kuwa ekoljia huweza kuishi bila binadamu lakini binadamu hawezi ishi bila ekolojia. Ni jasiri anapokabiliana na ndugu Kikwiro katika juhudi za kuondoa takataka kwenye lango kuu la Tikitimaji. Ingawa analetewa askari, wanakabiliana na askari hawa na kubuni njia mbadala za kuunadhifisha mji. Fasihi inapasa kuwasilisha nguvu ya lugha ya binadamu kuhusiana

na mazingira. Anafaulu kutukia lugha ya kusuta na kumkomesha. Anasimama kidete na kumwelezea ndugu Kikwiro maana ya mazingira yaliotunzwa. Anasema hivi:

> *Vundo la harufu lililotokea sehemu hiyo lilitishia hata kuiharibu sifa ya Tikitimaji. Sura hiyo inaweza kumfanya mgeni anayeingia Tikitimaji asipendezwe na anachokiona. Na wawekezaji wanaweza kususia Tikitimaji kwa sababu hiyo* (uk. 125).

Maya ni mhusika wa nne kati ya wahusika wakuu. Pia ni mtetezi wa mazingira na pia msimulizi mzuri wa hadithi. Ni msomi na alikuwa akifanya kazi kwenye maktaba ya mjini. Walipokuwa katika makao ya Quadulupe, aliwapiku wenzake katika utambuzi wa mambo ya kielimu. Ni kupitia sifa hii wanapokuwa safarini na wenzake anabainisha aina za ndege pamoja na majina yao. Katika ukurasa wa 26 anaeleza kuwa maji yanaendelea kukauka kwa sababu ya matendo ya binadamu. Kupitia kirejeshi nyuma, Maya anaonyesha jinsi hapo zamani mazingira yalikuwa yametunzwa na yalivutia. Mvua ilinyesha kila wakati na majani yenye kijani kibichi yalipendeka. Baada ya kuyarejelea matukio haya analinganisha na hali sasa na kusema kuwa ni matendo ya binadamu ndio yaliyoathiri mazingira.

Binadamu waliipukuta miti na kuweka majengo. Ndege walihama maskani yao. Maji yakahama na maji kuchafuliwa kiasi kwamba yalichuruzika kama lami. Anaeleza kuwa hali hii ni tofauti na hapo zamani ambapo maji yaliweza kuonekana na viumbe wake. Pia kutia jicho lake la uzinduzi, analinganisha uchafuzi wa mazingira na mjini ambapo viwanda vya mafuta vinatapika mabaki yake mle ndani:

> *"Sasa ni yale yale ya ule mto wa mjini. Viwanda vya mafuta vinayatapika masimbi yao mle. Watu wasiojali wanaumwaga*

*uchafu*

*wao humo," akasema Maya* (uk.89-90).

Pia anabaini kuwa chembechembe za risasi zilizotumiwa kwa njugu na mchuuzi ule, ziliweza kusababisha ugonjwa wa kansa.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), wahusika wakuu husaidiwa na wahusika wasaidizi kukuza msuko wa hadithi. Katika riwaya hii ya Tikitimaji, wahusika wadogo ni: mzeee Jududi, mzee Dhamiri, Jarisa ndugu Kikwiro, Jitikiti na mwalimu Insafu.

### 4.2.2 Mzee Jududi

Ni mtetezi wa mazingira. Hana kisomo cha kisasa lakini anayo maarifa ya jadi kuhusiana na uhifadhi wa mazingira. Katika ukurasa wa 37, anasimulia msitu Trimacho ulivyokuwa umetunzwa na jamii nzima. Anasema hivi:

> *...tangu jadi na asili, jamii yao iliishi kwenye msitu wa Mlima wa Trimacho. Ulikuwa msitu maarufu na uliokuwa na miti adimu sana- mingine hata haipatikani sehemu yoyote nchini. ...msitu ndio ulikuwa kila kitu chao na walijua jinsi ya kuulinda msitu wenyewe* (uk.37).

Msitu huo ulikuwa na miti adimu na pia ulikuwa na vianzo vya mito yote. Mzee huyu ni mwenye maarifa. Anawapa vijana wosia kuhusiana na masuala ya mazingira. Kwake anasema kuwa si hoja kuona mandhari mapya kama alivyodakia Sapna kuhusu mazingira mazuri, uk 36 bali ni kuangalia mazingira kwa jicho jipya na kutoa sauti. Kwake ni kupitia sauti za wahusika kwenye kitabu hiki ndipo mazingira hutoa sauti yao. Kinyume na utafiti wa Sabula(kt) mhusika huyu anawahimiza wanajamii wote kuangalia suala mazingira kwa jicho jipya. Jinsia zote zinahimizwa kuhusika katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira.

Katika masimulizi yake mwandishi anatufichulia athari ya matendo ya binadamu kwa mazingira. Anabainisha uhasama uliopo kati ya binadamu na mazingira; kukata miti

kwa ujenzi bila kupanda miti mingine, kuhama kwa viumbe vya bioanuai kutokana na mazingira yasiohifadhiwa na kuuza mazingira kwa watu wa kibinafsi. Anasema kuwa ulimwengu si wa binadamu pekee bali hutegemea mfumo mzima wa mahusiano.

#### 4.2.3 Mzee Dhamiri

. Ni mhamasishaji kuhusu mazingira. Katika uk. wa 95, anasema kuwa kila pahali ni Tikitimaji. Anabainisha tamaa ya binadamu inayompelekea kuua mazingira yake. Anasema kuwa ile falsafa ya undugu ilipotea na ikasalia falsafa ya kitu. Katika uk. 98 anasema kuwa uchafuzi wa mazingira umeenea. Anawauliza vijana kuwa ile sehemu waliotoka kama hamna matatizo kama yale. Katika uk. 99, anawakosoa vijana kwa kuwauliza walikokuwa wanaelekea ilihali wameacha Tikitimaji kule walikotoka. Kazi ya msanii inapasa kuwasilisha ukweli kama ulivyo katika mazingira yake (muhimili wa (a) wa uhalisia). Mzee Dhamiri ni mmoja wa wahusika ambaye anawaonyesha vijana hawa na umma kwa ujumla kuwa uhifadhi wa mazingira huanzia anamokaa mtu bali si ugenini.

Mzee Dhamiri pia ni mkombozi wa mazingira. Anawaeleza vijana kujichunguza wenyewe. Jamii ya kesho itabadilika tukijichunguza wenyewe, tuwe wepesi wa kujilaumu. Sauti ya vijana itasikika hata hivyo sauti hizo zitavilia ndani kwa ndani iwapo vijana hawa watarithi maguada yasiyofaa. Mzee Dhamiri ni mzee mwenye maarifa tele kuhusiana na masuala ya mazingira ambayo anawahimaza vijana kutumia katika kusuluhisha majanga ya mazingira. Anawapa vijana changamoto kuhusiana na maamuzi yao. Dhana hii inafafanuliwa na muhimili wa d) wa nadharia ya uhalisia ambapo wahusika ni vielelezo yakini wa binadamu wa kawaida kwa vile wao hutumia lugha ya kawaida kumwezesha binadamu kujifafanulia uwezo wake wa kutenda mambo. Kauli nzito za mzee huyu zinawawezesha vijana hawa kufanya maamuzi ya busara kuhusiana na uhifadhi wa mazingira.

### 4.2.4 Ndugu Kikwiro

Huyu ni waziri ambaye amesimamia masuala ya usafi. Si mtetezi wa mazingira kwa sababu anadidimiza shughuli za utunzaji wa mazingira.

*Akasema kilicho muhimu hakikuwa mazingira bali kitokanacho na mazingira yenyewe. Haijalishi hata kama mtu atayatia mazingira yenyewe kwenye kamuzi na kuyakamua kiowevu kilichoweza kukufaidi. Watu wamo mbioni kutafuta hela hakuna anayeshughuilika na asili au mazingira hayo ayasemayo.*

*Haijalishi kama mtu atayaua mazingira yenyewe au la. Ukiweza hata kuufukua utumbo wa mazingira ndio bora kabisa* (uk. 127).

Anasema kuwa haijalishi kama binadamu atayatia kitanzi mazingira yake mradi tu apate hela. Anasema kuwa mazingira si muhimu bali ni kinachotokana na mazingira hayo. Mazingira yapaswa kufukuliwa na kutoboa utumbo wake ili kupata hela. Kupitia kwake mwandishi anatoa mielekeo ya viongozi waliopewa mamlaka kulinda haki za mazingira jinsi wanavyoua mazingira. Fasihi ianapaswa kuwakilisha mielekeo ya binadamu kuhusiana na mazingira. Mwandishi amemwakilisha mhusika huya kihalisia kuhusiana na msimamo wake kuhusiana na mazingira.

Ni mbinafsi; Katika uk wa 127-128, anawapa akina Sapna na kundi lake la WAZALIMA ruhusa ya kushughulikia mlima wa taka lakini kwa mabezo na masharti kuwa wasiitishe malipo. Anapuuza uhifadhi wa mazingira kwa ajili ya urembo. Wanafanya njama ya kuficha stakabadhi muhimu katika chumba kimoja chenye uchafu. Fasihi mazingira hujihusisha na matendo ya binadamu na uhusiano wake kwa vitu

vilivyo hai na visivyo hai. Uhusiano wa mhusika huyu kuhusiana na vitu visivyo na uhai ni hasi. Havithamini kwani yeye huthamini hela.

### 4.2.5 Jitikti

Ni kingozi wa Tikitimaji. Amepewa majina mengi na mwandishi. Mhusika huyu amesawiriwa kisiasa na mwandishi. Amepewa majina; Durago, Stikilali, bepa wa soko na Dura. Majina haya aliyopewa ni ya kimajazi. Anauza mlima ambao ulihodhiwa na jamii kwa mujibu wa sheria za kitamaduni na kuifanya mali ya mtu binafsi. Katika uk 95, anaogopa kukumbushwa jana. Jana ambayo aliitia kitanzi kimazingira. Ananunua msitu wa Tirimacho katika uk 41.

## 4.3 Usawiri wa Wahusika Katika Kuwasilisha Maudhui Ya Mazingira Katika Riwaya ya Msimu wa Vipepeo

### 4.3.1 Mkurutu kama waziri wa utalii na mazingira

Waziri alipewa jukumu na serikali kuhakikisha kuwa mazingira yamehifadhiwa ipasavyo. Waziri huyu si mtetezi wa mazingira. Katika ukurasa wa 46, waziri anakutana na rafikiye Fabio Mkalla ambaye ni mwanasheria kuzungumzia kuhusu kuuzwa kwa makavazi ya kihistoria. Wanatumia mwanya uliopo katika kipengele cha katiba kuhusu *national monuments* wa kuipa mamlaka wizara ya utalii na mazingira ya kuiuza.

Mkurutu ni mwenye mapuuza hasa pale panapoibuka tetesi kuwa palikuwepo na meli ambayo ilikuwa imemwaga mafuta baharini. Wataalamu wa ekolojia katika ukurasa wa 99, walieleza kuwa mafuta ile haikutishia tu viumbe wa majini kama samaki na wengineo bali hata matumbawe yalioenea sehemu hiyo ambayo yalikuwa muhimu sana kama mbelewele ya kuwavuta nyuki wa utalii. Pia walikuwepo ndegendege kama membe na wengineo ambao walikuwa kwenye hatari kubwa. Tukio hili lingeweza kuepukika kwani kampuni iliyohusika na masuala ya mazingira, *Enviromental watch*

ilishikilia kwamba kampuni hiyo iiyohusika ilipe fidia ya kusaidia kukomboa mazingira.

Waziri Mkurutu hakujishughulisha na mjadala huo uliohusu wizara yake. Alipoitwa kwenye vyombo vya habari kutoa taarifa kuhusu tetesi zile, waziri Mkurutu alianza kulia na kusema kuwa haiwi kwenye kaida yake kulia lakini habari za uongo kama zile zilienezwa na mahasidi wake. Alijifanya kutoa machozi kadamnasi ya umma ilihali alipofariki mama yake hakutoa hata tone la machozi.

Katika ukurasa wa 101, alichukulia kuwa kulia ni dawa ya hadhira yake. Hakuwa mwadilifu kwenye kazi aliyopewa kama waziri wa mazingira. Mhusika huyu amesawiriwa na mwandishi kisiasa na alichukulia kazi aliyopewa kisiasa. Kwake siasa ni sanaa ambayo inapaswa kuigizwa. Alichukulia kuwa anapolia hadhira yake huwa imeigizwa na imetibiwa. Machozi ya waziri Mkurutu iliweza kusimamisha harakati za ukombozi wa mazingira. Mazingira yaliendelea kuchafuliwa na yeye akasalia kuwa msanii wa machozi.

Alianzisha mradi wa ufugaji wa vipepeo katika eneo bunge lake la Kisangu ambapo alitumia wadudu hawa kujinufaisha. Katika ukurasa wa 182:

*Wanaeneobunge wakajitosa kwenye msitu wa pale na kuwakusanya vipepeo wa aina tofauti tofauti kwa kutumia vitungi vidogo* (uk.182).

Viumbe hawa walitolewa kwenye mazingira yao asilia na kuwekwa kwenya mazingira mapya kwa minajili ya biashara. Katika ukurasa wa 206, kama alivyoelekezwa kwenye mradi ule wa ufugaji vipepeo, kunao vipepeo ambao waliweza kuadimika kutokana na ukosefu wa mimea fulani. Basi kunao uwezekano mkubwa sana kuwa ingawa waziri aliuanzisha mradi ule, palikuwa na uwezekano mkubwa sana wa kupotea kwa vipepeo ambao hawakupata aina ya miti au mimea ya kuwasitiri.

Waziri Mkurutu ni mbinafsi. Aliwadanganya wanaeneobunge kuwa mradi ule wa ufugaji wa vipepeo ni matunda ya utandawazi. Usemi huu haukuwa na ukweli wowote maanake mradi ule ulimnufaisha yeye tu. Katika mauzo ya vipepeo wale, aliwasili amechelewa na mvua kubwa ikanyesha. Lori ambalo lilikuwa limebeba pupa lilikwama matopeni. Aliitisha usaidizi wa gari lake tu bila ya kujali mali ya wanakisangu. Baada ya siku mbili gari lile lilikwamuliwa na kampuni baada ya kusubiri usaidizi wa wanajeshi. Katika ukursa wa 279, mwandishi anaeleza kuwa pupa walikuwa wamepasuka na vipepeo wasiokuwa na nguvu kutoka kwenye vimvugu vyao. Maisha ya viumbe hawa yalikuwa yamekatizwa kutokana na ubinafsi wa waziri huyu.

**4.3.2 Kanda**

Kanda ni mtetezi wa mazingira. Katika ukurasa wa 110, anatambua moshi mweusi uliokuwa umetanda jijini. Anasema kuwa moshi ule umekuwa tatizo kubwa pale jijini. Kupitia mbinu rejeshi, anakumbuka jinsi chama cha wanamazingira kilipojaribu kuwapeleka wenye viwanda mahakamani kwa malalamishi kwamba hawa wenye viwanda wameharibu mazingira yao lakini kesi hiyo ikafutiliwa mbali kwa kukosa ushahidi wa kutosha wa kisayansi. Garrard (2007) anaeleza kwamba matataizo ya kimazingira yanaonekana kimsingi kuwa matatizo ya kisayansi, katika muktadha huu ndiposa kesi hii inafutiliwa mbali. Baadaye kupitia simulizi za mhusika huu tunapata ushahidi tosha wa kuwepo kwa uchafuzi wa hewa. Msanii anaangalia matatizo na kuchunguza chanzo chake (muhimili wa (c) wa nadharia ya uhalisia) mabadiliko haya hayajakadiriwa kisayansi bali yamesawiriwa kupitia kwa mhusika Kanda.

Aling’amua mapendekezo yaliyotolewa na wanachama wa mazingira kuhusiana na waendeshaji magari. Waendeshaji magari walikuwa wamehimizwa kutumia dizeli ambayo haina salfa kwa sababu ilikuwa nzuri kwa mazingira. Lakini Kanda alitambua

kuwa hamna mtu aliyetilia maanani mapendekezo yale. Mapuuza yao ndio yaliyopelekea kutanda kwa moshi jijini ambao ulikuwa unatangaza kifo cha mazingira.

*Alisimama karibu na dirisha huku macho yake yametekwa na moshi mweusi uliotanda upande wa mashariki* (uk.110).

Ingawa ukarabati wa bomba la maji lilikuwa jukumu la manispaa ya jiji uk.13, Kanda aliwajibika na kulirekebisha bomba lile. Kanda hakuwa na kipato kikubwa kifedha lakini alijitahidi kutengeneza bomba. Alitumia mipira kuukuu kisha akaomba vipuli vya kufungia bomba lile lisimwage maji. Bomba hili lilikuwa tayari limeanza kutengeneza kidimbwi cha maji chafu na kama si uwajibikaji wa Kanda basi maeneo haya yangekuwa tatizo kwa maisha ya watoto waliokuwa wakichezea pale. Mhusika huyu anadhihirisha kuwa uhifadhi wa mazingira hauhitaji kiasi kikubwa cha fedha bali moyo wa kujitolea kwa shughuli yoyote ya kimazingira inayotokea. Kama ilivyo katika mhimili wa kwanza wa nadharia ya uhalisia, fasihi inapaswa kuwasilisha ukweli kama ulivyo katika mazingira yake. Mazingira anayoelezea Kanda yanaakisi hali halisi katika maisha ya binadamu.

### 4.3.3 Kalulu

Ni mwandishi wa habari katika gazeti la kibinafsi. Ni mwandishi mashuhuri na mkombozi wa mazingira kupitia vyombo vya habari. Katika ukurasa wa 116:

*"Safari yao ya kwenda Kishela iliwatibukia pakubwa baada ya kukumbana na Gattuso Berlusconi ambaye alikuwa kwenye boti lake la mbio akilinda ghuba yake isiingiliwe na wavuvi wa kisiwandeo* (uk. 116).

Kalulu na mpiga picha John Ogolla wanakabiliwa vikali na Gattusu Berlusconi katika kisiwa cha Kisiwandeo. Kalulu alizuru kisiwa kile kupata ukweli kuhusu umwagaji wa mafuta katika bahari. Ni mwandishi asiyesaza habari muhimu. Anatumia maarifa yake yote kupata ukweli kuhusu uchafuzi wa maji baharini pamoja na kubaini chanzo cha

kupungua kwa samaki kisiwani. Ili kupata habari hizi, anakabiliwa vikali na Gattusu Berlusconi hali iliyopelekea kuuliwa kwa dereva wao. Mwandishi amemtumia mhusika huyu kuonyesha kuwa harakati za ukombozi wa mazingira huambatana na changamoto nyingi sana ikiwemo kupoteza kwa maisha.

### 4.5.4 Guttasu Berlusconi

Kupitia utandawazi, huyu ni mwitaliano ambaye anatumia istilahi hii kumaanisha utandawizi anamiliki ufuo wa umma na kuwanyima wenyeji fursa ya kuhifadhi na kutunza. Kilabuko na Madete (2010), wanasema kuwa uchafuzi wa hewa hupunguza viumbe vya bioanuai. Wanaendelea kusema kuwa vichafuzi hivi vya hewa kuangukia uoto mbalimbali na kupunguza idadi ya mazao katika sekta ya kilimo. Katika ukurasa wa 65, tunaelezwa kuwa:

*Kalulu alikuwa akimalizia ripoti yake kuhusu lile trivyogo lililowalaki kisiwandeo ambalo lilitokana na tabia ya mwitaliano aliyefahamika kama Berlusconi; aliyewakataza wavuvi kuvua kwenye ufuo uliokuwa karibu na jumba lake kubwa kwenye mtaa wa kishela (uk.65).*

Anamiliki ghuba ya samaki wengi. Anawavua samaki hawa bila kuchagua wala kujali idadi yao. Anakabiliana vikali na yeyote aliyekaribia ufuo huo. Mhusika huyu amesawiriwa kiuchumi na mwandishi kutoa uhalisia uliopo baina ya binadamu na uhifadhi wa mazingira kwa ajili ya uchumi. Lililo muhimu kwake ni kuendelea kufaidika na viumbe asili bila kujali mahitaji yao. Kama anavyosema Dean (2002) kwamba uwazi wa kibiashara kimataifa umechangia pakubwa uchafuzi wa mazingira kwani kanuni zinazoendesha biashara kama hizi huwa legevu sana. Mara nyingi uwazi huu wa kibiashara huegemea tu faida kifedha. Mwitaliano huyu ni kama amenyakuwa ufuo huu ambao uliwasaidia wenyeji hawa.

### 4.3.4 Mzee Kitali

Huyu ni mhusika msaidizi. Katika ukurasa wa 62, anatambua umuhimu wa malighafi itokanayo na uhifadhi wa miti ainati katika jamii anamweleza Julia hivi

*"Hatukuchemsha mzizi ya mgunga, kuichemsha na kukunywesha? Je, ulipochibuka ukicheza; ulipojikata ukiwa shuleni na hata kuwa na vidonda hatukutumia maji ya mshubili? Je, babangu mwenyewe aliposhikwa na shinikizo la damu nahata kuvimbiwa hatukutumia maji ya mdalasini? Je mamako alipokuwa mjamzito hakula terere na manage kuimarisha damu yake?* (uk.62)

Anatambua tiba ya maradhi mbalimbali; tiba ya maradhi ya tumbo kuwa mizizi ya mgunga, dawa ya kuchubuka ngozi na kuwa na vidonda kuwa ni maji ya mshubili, shinikizo la damu tiba yake ni maji ya mdalasini na mwisho mboga za kienyeji kama vile terere ziliafiki mama mjamzito na kumpa afya nzuri. Mzee huyu aliamini kuwa binadamu hawezi kamwe kuishi bila dawa hizi za kienyeji zilizotoka kwa miti mbalimbali. Ni mhusika ambaye anaamini kuwa afya ya binadamu huimarishwa kwa kutumia miti. Ndipo miti hii mbalimbali ipatikane kwa ajili ya shughuli hii ni lazima mazingira yalindwa na kuhifadhi spishi mbalimbali za miti hii. Ni mhusika ambaye anaeleza umuhimu wa kutunza mazingira kwa kuelezea wasomaji umuhimu wa miti. Ingawa anapuuza ukuuwaji wa sayansi na technolojia katika kusuluhisha magonjwa mbalimbali anapeana njia mbadala za kusuluhisha magonjwa haya.

### *4.3.5* Fabio Mkalla

Huyu ni mhusika msaidizi ambaye amesawiriwa na mwandishi kisiasa na kiuchumi. Ni mwanasheria ambaye anatumia maarifa yake ya sheria kupuuza mstari mdogo kwenye sheria za nchi ili kunyanyasa mazingira., Anasema kuwa:

"*Sidhani. Ni mstari mdogo kwenye sheria za nchi; unaweza hata kupuuzwa. Lakini kipo kipengele kinachoipa wizara ya Utalii na Mazingira mamlaka makubwa!"* (uk.46)

Katika usemi huu, Fabio anatumia maarifa yake kumkn abidhi Dieter Adolf jengo hili lililomilikiwa na jamaa za mshairi maarufu wa zamani. Mhusika huyu anawakilisha viongozi waliona ushawishi. Kama anavyosema Wallace (2009) kuwa mazingira hayarejei tu mazingira asilia bali pia huhusisha mandhari yaliojengwa na binadamu na mitaguasano ya elementi asilia na utamaduni. Mandhari aliyojenga dieter yana athari hasi kwa mazingira na utamaduni wa wananchi hawa. Huyu ni mhusika aliye na ushawishi katika jamii na anatumia mamlaka yake kuweka kanuni inayoidhinisha unyakuzi wa majengo asili yanayohifadhi utamaduni wa mazingira.

## 4.4 Uchanganuzi wa lugha kitamathali Katika Riwaya Ya Tikitimaji katika kuwasilisha masula ya mazingira

### 4.4.1 Matumizi ya tashibihi

Wamitila (2003), anatoa maaana ya tashibihi kwa kusema kuwa ni tamathali ya usemi ambapo vitu viwili hulinganishwa kwa njia ya moja kwa moja. Mohammed (1995), naye anasema kuwa msingi wa tashibihi hufuata namna ya kuweka wazi maana, dhana na picha fulani kwa mujibu wa kiulinganifu wa picha. Tashibihi hutambulishwa na matumizi ya maneno kama vile; kama, mfano wa, mithili ya, kama vile, sawa na n.k.

Katika ukurasa wa 5, msimulizi anatumia tashibihi ifuatayo:

> *"Tulikaribishwa Quadulupe na ule ubaridi unaosababishwa na miti mingi iliyopazunguka. Ile miti mirefu ilikuwa ikicheza huku na huku kutokana na upepo uliokuwepo. Harufu ya mimea, sauti nzuri za ndege na upepo mwanana vilitupiga pambaja kubwa. Tukahisi kama mtoto aliyebebwa juujuu na mzazi wake anayezunguka huku na kule"* (uk.5).

Ulinganisho huu unatokana na ari ya mwandishi kutaka kuelezea hadhira yake kuhusu faida za utunzaji wa mazingira kwa afya ya binadamu. Katika ukurasa wa 23 mwandishi anatumia mbinu hii ifuatavyo:

"*Mizizi ya mimea iliyokuwa juu ilijitokeza kama matanzu ya mgunga mweupe" (*uk.23)

Mwandishi anaelezea kuwa mizizi ya miti ilijitokeza kama matanzu ya mgunga mweupe. Ulinganisho huu wa mizizi ya miti na matanzu ya mgunga mweupe waweka wazi suala la mmomonyoko wa udongo. Ni bayana kuwa hakuna dalili zozote za uhifadhi wa ardhi. Pia mandhari kama haya yana hatari kwa maisha ya binadamu; aidha wapitia njia huhatarishwa na miti iliyoelea njiani. Mzee Jududi anapojiandaa kuwasimulia vijana: Maya, Kombo, Sapna na Zinji, anatumia tashibihi ifuatayo:

*"Mzee Jududi naye akapumua kama hamali aliyejiandaa kulibwata gunia lililomlemea mabegani".*

Mzigo unaoelezewa kupita tashibihi hii ni matatizo waliyoyapitia watu wa nchi ya Tikitimaji. Huu uzito unalinganishwa na uzito wa roho yake anaporejelea makovu haya. Makovu haya yanarejelea kufurushwa kwa wenyeji kutoka mlima wa Trimacho na Jitikiti ambaye sasa alikuwa kiongozi. Mlima huu unauzwa na kumilikiwa na Durago. Kihistoria jamii ziliishi kwenye mlima huu na kutunza ipasavyo maliasili hii. Hii inatokana na kauli kuwa uhifadhi wa mazingira ni jambo la lazima na la jamii nzima.

Pia kupitia tashibihi hii, mzee Jududi anaeleza jinsi zamani nchi ya Tikitimaji ilivyofunikwa na blanketi nzito la kijani na jinsi hewa ilivyokuwa safi. Ni wazi kuwa kulingana na mpito wa wakati pamekuwepo na mabadiliko ya mazingira. Katika ukurasa wa 44, mzee Jududi analinganisha hali ya zamani na sasa ambapo hewa ilikuwa tofauti

*"Hewa ya harufu ya kijani iliburudisha ilipoingia kwenye mianzi ya pua. Mtu unatamani uendelee kuivuta ndani hewa hii na kupata nguvu mpya. Sio sasa ambapo hewa inayoingia mwilini ina joto na inasikika kama ina vumbivumbi. Unatamani kuitoa nje kama tapishi"(u.k 44.)*

Ulinganisho huu wa hewa chafu na yenye joto na vumbivumbi na tapishi unadhihirisha athari ya uchafuzi wa hewa kwa afya ya binadamu. Mazingira yamechafuliwa kiasi cha kwamba yasiweze kumsitiri adinasi kwa ustaarabu wake. Maelezo haya yanalingana na ripoti ya IPCC ya (2014) ambapo ilisema kuwa kwa miongo miwili ya karne ya ishirini ilikuwa yenye ongezeko la joto hewa na athari chafu ya hewa. Hii athari chafu ya hewa ndio imeelezwa hapa na mzee Jududi jinsi inayoathiri maisha ya kawaida ya binadamu. Mwandishi mara nyingi hutumia lugha ipasavyo ili kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake. Kwa kutumia tashibihi, msomaji anajenga taswira ya hewa haswa taswira ya mnuso. Masuala ya mazingira yamebainishwa na tashibihi hii.

Mbinu hii pia inajitokeza katika ukurasa wa 88, mwandishi anaeleza hivi *"Wimbi kubwa la harufu ya uozo likawa nusura kutuzoea na kutupeperusha juu kama usufi uliosombwa na chamchela*."(uk.88)

Harufu kali na yenye mnuso wa uozo inanuswa na wahusika hawa wakuu: Sapna, Maya, Kombo na Zinji kutoka hatua mbali kuelekea mji wa Tikitimaji. Ukali ndani ya pua ya Sapna ambalo limelinganishwa na wembe, ndiyo uliobainisha harufu hiyo. Kadri walivyosonga ndivyo harufu ilivyoendelea kuongezeka.

Mazingira yalikuwa yamechafuliwa na uvundo huo ulikuwa umeenea kote. Wanakijiji nao walikuwa wameuzoea uvundo huo. Maelezo hayo yanaendana na maelezo ya Reuveny (2007) aliposema kuwa watu huweza kuliangalia suala hili la mazingira kwa njia tatu ambapo njia mojawapo kati ya hizi tatu ni kuketi mahali pale pachafu bila kufanya juhudi zozote za kupasafisha mahali hapo. Hii inabainishwa na kauli ya vijana ambao walikutana na wahusika wakuu ambao walioonekana kusumbuliwa na harufu hiyo ya uvundo.

Matumizi mengine ya tashbihi ni:

"*Baada ya muda mfupi kundi la WAZALIMA likawa na wanachama wengi. Kundi lenyewe lilikuwa kama chavua inayovuta nyuki na wadudu wengine"*. (uk. 128)

Chavua ina punje ndogo ndogo ambazo hutokezwa na viungo vya uzazi vya kiume katika mimea inayotokeza maua au sonabari. Mimea hutoa chavua ili iweze kuzaa. Ulinganisho huu ni wa kuleta mabadiliko. Sapna ndiye aliyeanzisha kundi hili la vuguvugu la WAZALIMA ili kuzoa taka na kuonyesha watu kuwa ule uvundo na taka huweza kuondolewa kwa jinsi hiyo na mazingira yakanadhifishwa. Sapna aliwahamasisha wanajamii hali iliopelekea uanachama wa idadi ya juu. Lengo ni kwamba binadamu asiwe kiumbe mnyamavu kuhusiana na masuala ya mazingira. Kwa mujibu wa mhimili wa (d) wa nadharia ya uhalisia, wahusika ni vielelezo yakini vya binadamu wa kawaida kwa vile wao hutumia lugha ya kawaida kumwezesha mwanadamu kujifafanulia uwezo wake wa kutenda. Mwandishi amejitahidi kuteua tashibihi mwafaka katika kuendeleza mawazo yake kuhusu masuala ya mazingira.

**4.4.2 Methali**

Kwa mujibu wa Finnegan (1990), Matteru (1987), Mulokozi (1989), King'ei na Ndalu (1989) na Maitaria (1991), wanakubaliana kuwa methali ni matamshi yanayosheheni hekima na ambayo huwasilisha ujumbe wake kitamathali. Mwandishi au msanii ana uwezo wa kubadilisha mwendelezo mradi tu maana isalie kuwa ile asilia. Mtunzi huteua methali na kuisarifu katika muundo wake. Huweza akapangua muundo wa methali hiyo na ikatumika kwa njia tofauti. Kulingana na maoni ya Saussure na Jackobson (1974), wanasema kwamba muundo na maana ya methali ni mambo yanayofanana.

Mulokozi (1996), anasema kuwa methali huwa na sehemu mbili kimuundo. Sehemu ya kwanza ambayo ndiyo hubeba wazo fulani na sehemu ya pili ambayo huwa na majibu au matokeo au ukamilishwaji wa wazo hilo. Mfano:

| **Wazo** | **ukamilishwaji** |
|---|---|
| Haraka haraka | haina Baraka |
| Mwenda tezi na omo | marejeo ngamani |
| Mpanda ovyo | hula ovyo |

Pia kuna kuna matumizi ya mbinu za kisanaa katika uundaji wa methali. Kuna matumizi ya stiari na ukinzani uitwao ukweli-kinzani. Mtano:

| **Hali** | **ukinzani** |
|---|---|
| Amani haiji | ila kwa ncha ya upanga |

Zipo njia kadha zinazoelezea muundo wa methali kama wanavyosema Mtesigwa (1989) na Mulokozi (1999). Wametaja baadhi ya mbinu hizi kama: matumizi ya kejeli kwenye methali kama mfinyanzi hulia gaeni, tashibihi mfano ujana ni moshi hufuka na kupotea, balagha na takriri. Muundo wa methali ni uhodari wa kutumia lugha kwa mvuto na kwa ufupi.

Methali hueleza maana dhahiri (maaana tumikizi) kama anavyosema Sengo (1979) na maana batini (lugha dhahania). Methali zina uwezo wa kuwasilisha maana nyingi za kijumla kuliko tamathali nyinginezo. Maoni haya ni sawia na Wamitila (1997) anayesema kuwa methali huwa na sifa ya wingi hali na wingi dhamira. Anasema kuwa sifa hii ilitambuliwa na wana-paremiolijia. Methali moja huweza kutumika kueleza maana tofauti na dhamira zake huweza kuwa nyingi. Maelezo haya yatatuafiki katika ubainishaji wa umbo la methali pamoja kuelewa maana na dhamira ya methali.

Mzee Jududi katika uk. 34, anatumia methali

*"Mgeni njoo mwenyeji apone*" (uk.34).

Anarejelea methali hii baaada ya wahusika Sapna, Maya, Kombo na Zinji kufika maeneo yale kwani iliaminika kwamba huenda wangeyatatua matatizo ya Tikitimaji. Matatizo ambayo yanarejelewa ni kuhusiana na umiliki na uhifadhi wa msitu Trimacho.

Jududi na wengine walifurushwa kutoka msitu huu na wageni ambao wao waliwakaribisha na wageni hawa kujinyakulia ardhi hii ambayo ilikuwa rasilimali muhimu kwa maisha yao. Methali hii inabainisha maudhui ya unyakuzi wa ardhi na misitu ambayo ilihifadhiwa na jamii kwa manufaa yao na kupokezwa kwa mtu binafsi ambaye hakujali maslahi ya wanajamii wengine. Pia methali hii inarejeleasuala la utunzaji wa mazingira. Mazingira yalitunzwa na wanajamii. Palikuwepo uhusiano mkubwa sana kati ya mazingira na utamaduni wa jamii hii.

Methali, *"penye njia milango i papo"* katika ukurasa wa 46, inamaanisha kuwa chombo kikikabiliwa na mawimbi makali huwa kinakaribia njia au milango ya kuingia bandarini. Mzee Jududi anatumia methali hii kuwatia moyo vijana hawa. Hii ni baada ya kuzungumzia hali mbovu ya mazingira anaposema kuwa binadamu wenyewe wanayatia kitanzi mazingira. Vijana hawa hawafi moyo. Sapna na Zinji wanajishughulisha na mapambano dhidi ya uchafuzi wa mazingira kwa kuandaa maandamano kuandikia habari hizi magazetini. Hawafi moyo bali wanaendeleza vita hivi kwa nguvu mpya. Huu ndio ushauri wanaopewa na mzee Jududi kuwa muda uliosalia wa kufaulu ni mfupi kwani wanakaribia ukingo. Kufaulu huku kunadhihirika wakati vuguvugu la WAZALIMA linaanzishwa na linafaulu kuondoa rundo la takataka.

Katika uk. 48 methali:

*"Paliwapo nyoka hapaachi ndomezi" (*uk.48).

Maana ya methali hii kwa mujibu wa mwandishi wa riwaya hii ni kuwa watu walikuwa na matatizo mengi yakiwemo yale ya ukosefu wa lishe ya mifugo yao. Ni kutokana na matendo yao ndipo lishe inaadimika. Ndomezi hii inatokana na athari ya kutotunza mazingira. Mto Unasi unatishia kukauka. Kama anavyoelezea mwandishi ni kuwa maji yalikuwa yamepungua kiasi kwamba majabali ndani ya mto yalionekana kulaliana. Hali hii ndio inayozua uhasama kati ya binadamu na mazingira. Kama anavyosema Wamitila

(2007) katika kufafanua nadharia ya uhalisia kuwa fasihi ni lazima ionekane kama kioo cha jamii. Hivyo basi ni lazima jamii iweze kujitazama na kujiona kupitia fasihi. Methali hii inaonyesha athari ya matendo ya binadamu kwa mazingira.

Methali *"kilio huanza na wafiwa ndipo wa mbali wakaingia"* katika uk. Wa 124 inatupa mwanga kuhusiana na suala la kutowajibika kwa viongozi haswa wale waliopewa nyadhifa za kusimamia na kutetea mazingira. Tikitimaji ni mfano wa nchi isiyojali mazingira yake. Ndugu kikwiro ambaye aliteuliwa kusimamia mazingira, anawaalaumu wenyeji wa eneo hilo huku akisahau kuwa takataka yenyewe ilikuwa kwenye lango kuu la kuingia Tikitimaji ambapo kila mgeni aliyeingia kupitia lango kuu hili alikutana na rundiko hili la taka. Kwa ukawaida wa sheria za baraza la jiji, jukumu la kuzoa taka limetwikwa baraza la jiji. Garrard (2004), anaangalia mipaka iliyoko ya ubinadamu na uso ubinadamu. Ni kweli kwamba wanatikitimaji wangekuwa mstari wa mbele kuondoa uchafu ule kwenye lango kuu, huu ndio ubinadamu.

Sapna alifanikiwa kuanzisha kundi la walinda usalama linalopata wanachama wengi ajabu. Juhudi hizi za kutafuta wanachama zinafaulu mwandishi anapotumia methali *"haba na habahujaza kibaba" (uk 12*) Juhudi zake zilianza kwa hatua chache lakini mwishowe alifanikiwa. Juhudi hizi zilizaa matunda kwani kundi hili lilifanikiwa kuwahamasisha wanajamii kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira na mchango wa kila mwanajamii katika shughuli nzima ya utunzaji wa mazingira. Vuguvugu hili linafaulu kubomoa mlima wa taka ambamo Jarisa na vijana wengine wa mitaani walizoea kuchakura kwa mahitaji yao ya kimsingi.

Methali imetumika kama chombo cha mapinduzi ya jamii kuhusiana na suala la mazingira. Marwa (1997) anasema kwamba methali hutumika kama chombo chombo cha mapinduzi kwa kuwa hujenga na hukusudiwa kuibuwa hisia za umma ili kuunga mkono au kupinga mambo mbalimbali.

### 4.4.3 Tashihisi/uhaishaji

Ni hali ya kunafsisha vitu, kuvifanya kuwa na maumbile na kusema kama mtu. Senkoro (1982), anaelezea tashihisi kuwa ni tamathali ya usemi ambayo wakati mwingine huitwa tamathali ya binadamu. Naye Kahiga (1995), anaeleza kuwa tashihisi ni tamathali ya usemi ambayo sifa ya uhai huwa imehamishwa kwenye kitu kisicho cha uhai au dhana dhahania. Kwa mujibu wa waandishi hawa ni dhahiri kuwa tashihishi ni tamathali ya usemi inayohusisha viumbe au vitu na sifa za binadamu.

Mwandishi anatumia tashihishi katika ukurasa:

*"Tulikaribishwa Qwadulupe na ule ubaridi unaosababishwa na miti mingi iliyopanguka. Ile miti mirefu ilikuwa ikicheza huku na kule kutokana na upepo uliokuwepo. Harufu ya mimea, sauti nzuri za ndege na upepo mwanana vilitupiga pambaja kubwa"* (uk.5)

Kuelezea hali ya hewa, baridi, miti na upepo. Anasema Ishara ya kuonyesha mazingira yaliyotunzwa na kuhifadhiwa vyema. *"Juzi na jana huzaa leo"* tashihisi hii inakuza maudhui ya mazingira. Matendo yetu kuhusiana na mazingira sasa yaani kwa wakati huu na mpito wa wakati kihistoria ndiyo hutupa ithibati iwapo tumeyahifadhi mazingira au la, pia inaashiria iwapo kuna mabadiliko katika utunzaji wa mazingira.

Mwandishi ametumia tashihisi hii kuonyesha uharibifu wa mazingira ambayo ndiyo dhamira kuu. Zinji, Sapna, Maya na Kombo wafikapo Ganjoni, msimulizi anaelezea hali ya hewa iliyokuwa tofauti na ile walioizoea. Hewa hii ilikuwa na joto fulani. Unyevunyevu wa eneo hili ulikuwa wa juu:

*"Hewa ya hapa ilikuwa tofauti sana na hewa tuliyoizoea. ilikuwa na joto fulani. Unyevu hewa wa eneo hili ulikuwa wa juu. Harufu yake ilikuwa mseto wa vumbi na majani yaliokauka. Hapa na pale upepo ulijaribu kuyazoa majani ambayo yalikatalia chini kuisusia safari hiyo ya lazima"* (uk. 17).

Katika ukurasa wa 24, upungufu wa maji katika mto Unasi unabainishwa na tashihishi ifuatayo:

*Majabali makubwa yaliyolala kwenye sakafu ya mto wenyewe yalidhihirika wazi* (uk.24)

Majabali haya yamehaishwa na kupewa sifa ya binadamu ya kulaliana kuonyesha upungufu wa maji yalioacha majabali haya wazi. Baada ya binadamu kugeuka na kuwa mchwa, waligeukia miti. Nyuki nao walitambua majira ya mazingira wakaanza kuhama na kuacha mizinga yao mitini. Mwandishi anaeleza athari hii ya mabadiliko ya mazingira na tashihishi ifuatayo:

*"Mizinga yao iliyokuwa imeangikwa mitini ikabakia ikienda miayo*" (uk 45).

Mizinga hapa imehusishwa kiasi kwamba inabainisha matendo ya binadamu kwa viumbe wengine haswa katika mfumo wa utegemezi katika mazingira. Kama anavyosema Chegbuy (1998), kwamba ekolojia yetu imo kwenye hatari ya maangamizi kutokana na matendo ya kibinafsi ya binadamu. Mwandishi ametumia mbinu hii kitaswira kuonyesha jinsi nyuki viumbe wadogo wanavyotambua mabadiliko katika mazingira ilihali binadamu hawawezi.

Mbinu hii imetumika kwa mapana na marefu. Katika ukurasa wa 26 mwandishi kupitia mhusika sapna anahaisha mazingira ifuatavyo:

*"Hata! Haya ya maji kukauka mtoni tunayasababisha wenyewe! Vitendo vyetu vinasonga koo mazingira yenyewe! Na tukiendelea hivi kiwiliwili cha mazingira kitasakamwa hadi kitoke gamba"*

Mazingira yamepewa uhai na mwandishi kupitia mbinu hii. Koo ya mazingira imebanwa na kwa hivyo ule uwezo wa mazingira kuhifadhi binadamu na viumbe wengine basi huenda ukakosekana. Kama wanavyosema Glotfelty (1996), Greenblatt (1992) na Beul (1995), kuwa binadamu hawezi kuishi bila ekolojia bali ekolojia huweza

kuishi bila binadamu. Basi ni kutokana na matendo ya binadamu ndipo ekolojia huathirika kwa namna hasi. Kauli inayoshadidiwa na ripoti ya IPCC (2013) inayofafanua kuwa ekolojia yetu imo hatarini kutokana na matendo ya kibinafsi ya binadamu. Pia wanachambua mihimili ya nadharia ya fasihi mazingira kwa kuangalia viwango vya mpangilio wa kibiolojia wa viumbe asilia na uwezekano wa ekolojia kustahimili matendo ya uchafuzi. Ni dhahiri kuwa ekolojia haiwezi kustahimili vichafuzi.

**4.4.4 Nidaa**

Nidaa ni usemi wa mawasiliano au sauti ya mshangao aitumiayo msanii kudhihirisha maoni yake ya hisia (Mugambi, 1992). Naye Senkoro (2011) anafasili nidaa kuwa msemo unaoonyesha kushangaa au kushangazwa na jambo fulani. Kwa ufupi kulingana na maoni ya waandishi hawa wawili ni kuwa nidaa ni usemi wenye kuelezea hisia fulani za mwandishi au mhusika katika kazi yoyote kutoa hisia za ndani kama vile huzuni, furaha, kughadhabika, au kushangazwa. Matumizi ya nidaa huteuliwa kulingana na hisia teule anayotaka kuwasilisha mwandishi. Kulingana na Wamitila (2008), ni matumizi ya siyahi au maneno ya kuweka wazi hisia kama vile huzuni, masikitiko na mshangao kutegemea kile anachotaka kuwasilisha.

Katika ukurasa 37, *"Ndiyo walifika watu!"* ni nidaa ambayo imetumiwa na mwandishi kuonyesha hisia za kusikitika na kujuta. Baada ya kuwakaribisha watu hawa na hata kuwaonyesha utamaduni wao, wageni hawa ndio walikuwa chanzo cha kupotea kwa msitu wao uliokuwa umetunzwa. Mbinu hii pia imejitokeza katika ukurasa wa 44:

"*Tulia hasa! Lakini hakuna aliyesikia kilio chetu! Wale waliipukuta miti yote na kuliacha eneo hili kama ulivyoliona!* (uk.44).

Mwandishi anatumia mbinu hii kuteka hisia za msomaji. Mwandishi anaeleza suala la uchafuzi wa mazingira kwa hisia nzito ambayo msomaji hatatamani kuyaharibu

mazingira yake yawe na sura sawa na yale yaliyoelezewa na mwandishi. Athari ya mbinu hii ni kuwa msomaji atajibiidisha kuyatunza mazingira yao. Kwa kweli wanatikitimaji waliamua kuzikubali changamoto za majanga ya kimazingira baada ya kuona kwamba hakuna aliyeshughulika na mazingira (Reuveny, 2007). Pia muhimili wa nadharia ya fasihi mazingira unasisitiza nafasi ya mitindo ya lugha na namna mitindo hiyo huathiri namna binadamu anavyotagusana na mazingira. Mtindo huu wa nidaa unaonyesha hisia za mhusika huyu za kuchoshwa na uharibifu wa mazingira.

Katika ukurasa wa 54, mbinu hii ya nidaa imetumika.

"*Tikitimaji iko kila pahali kwa kweli! (uk.54)*

Suala la uharibifu wa mazingira limeenea kote kote. Mzee Jududi anatumia nidaa hii kuwahamasisha vijana hawa; Sapna, Maya, Kombo na Zinji. Hali hii inabainika na hatua alizochukua Sapna na vuguvugu lake kunadhifisha miji hata huko mjini.

Mbinu ii hii pia inajitokeza katika uk wa 127:

*Sapna akashusha pumzi kabla ya kuendelea, "ofisa huyo…ofisa kama wewe tu, akasema kuwa tukio hilo lilimfundisha jinsi ya kuwaza kama mlima. Hatupaswi kuyawazia matakwa yetu Bali pia ya ulimwengu wa asili. hatuishi tu sisi, yanaishi mazingira pia!"* (uk.127)*)*

Kupitia mbinu hii ya nidaa, mwandishi anatoa hisia za wahusika kuhusiana suala nzima la mazingira. Kama unavyosisitizaa muhimili wa fasihi ekolojia kuwa ni lazima mitindo zinazoteuliwa na mwandishi wa fasihi zionyeshe jinsi binadamu anavyotagusana na mazingira, basi mbinu hii inaoyesha hisia za binadamu kuhusiana na mazingira. Ubinafsi uliowajaa binadamu unathibitishwa na mbinu hii. Ni baini kuwa mazingira na binadamu huchukuwa nafasi sawa katika mfumo wa upangaji wa bioanui.

### 4.4.5 Kuchanganya ndimi

Muysken (2000), anafafanua kuchanganya ndimi kuwa mazingira yoyote ambapo kipengele kimoja cha kileksika na sehemu ya kisarufi kutoka kwa lugha mbili tofauti hujumuishwa pamoja au hutokea pamoja katika sentensi moja. Naye Grusjean (1992) anasema kwamba kando ya kufidia msamiati, mbinu hii hutumika sana katika kunukuu neno alilosema mhusika au kundi fulani la watu katika kuelezea matukio yaliotendeka kihistoria. Nao Bhatia na Ritchie (2004) wanafafanua kwamba kuna lugha ambazo zimehusishwa sana na jamii fulani, mada fulani, tabaka, dini na jinsia, umri na maarifa ya kijamii na lugha hizi zinapotumiwa katika hali ya kuchanganya msimbo basi hukuza sifa za wahusika. Pia kuchangaya ndimi ni njia mjawapo ya kuunda au kuharibu uhusiano uliopo baina ya wanakundi. Huweza kuharibu, kuchochea au kubadilisha uhusiano baina ya wanachama (Gal aliyenukuliwa na wardhaugh2002).

Katika ukurasa wa 46, mwandishi anaeleza hivi:

*"Na nyie hamlalamiki?" akauliza mzee Jududi. "Sana! Sapna ambaye ni mwanamazingira ameongoza maandamano mara ngapi? Sapna aliyaita nini? "Mahatma Gandhi aliyaita satyagraha!" alisema* (uk. 46).

Neno *satygraha* limetumiwa. Neno hili ni la kihindi linalomaanisha maandamano ya amani. Neno hili limetumiwa mbadala kuufidia msamiati mwafaka wa kuelezea hali ya ukombozi wa mazingira. Masuala haya ya ukombozi wa mazingira ndiyo yalioangaziwa katika nchi ya India katika enzi za Mahtama Gadhi. Sapna ambaye ni mwanamazingira anaongoza misururu ya maandamano *(satyagraha*). Katika riwaya ya Tikitimaji, sapna anashurutisha wale wanaohusika na utunzaji wa mazingira kukoma kukata miti na kuchafua mito.

Neno hili pia linatufafanulia nafasi ya viongozi katika utunzaji wa mazingira. Ndugu Kikwiro kama kiongozi anayesimamia wizara ya utunzaji wa mazingira anapendekeza

kuwa uchafu utupwe mtoni. Neno hili pia limetumiwa kuelezea maandamano yaliyofanywa na Maya kupinga uharibifu wa mazingira. Neno hili linaashiria juhudi za ukombozi wa mazingira katika riwaya. Pia limetumika kuleta pamoja wanachama na kuchochea juhudi za kuleta mwamko mpya katika utunzaji wa mazingira. Muhimili wa fasihi ekolojia wa hunuia kuleta mageuzi ya kimazingira kupitia fasihi unathibitika kutumia mbinu hii ya kuchanganya ndimi. Pia mbinu hii inathibitisha muhimili wa fasihi ekoloji unaosisitiza uwezo wa lugha katika kuwasilisha masuala ya mazingira.

**4.4.6 Misemo**

Ni fungu la maneno ambalo hutumiwa na wanajamii kwa namna maalum ili kutoa maana (Kiango & Mdee, 1995). Nao Kiribi, Nyonje & Wandeo (2007), wanasema kuwa misemo ni kauli fupi zinazoeleza ukweli fulani kwa kutumia tamathali za lugha na taswira. Kwa mujibu wa fasiri za waandishi hawa ni kuwa misemo ni kauli zinazotumiwa katika mawasiliano ili kutoa ukweli fulani kuhusu jambo na ukweli huo haujitokezi wazi bali kwenye ufiche fulani.

Katika riwaya hii ya Tikitimaji, mwandishi ametumia misemo mbalimbali kama inavyojibainisha. Katika ukurasa wa 39, *msemo angua kicheko* umetumiwa kutoa ukweli kuhusu kuuzwa na mlima Trimacho. Pia katika ukurasa wa 45 mwandishi anaeleza kukosekana kwa matumaini kwa wanatikitimaji baada ya mazingira kuharibiwa. Hali hii ilipelekea nyuki kuhama.

*"Wanatikitimaji walikata tamaa na kupasua mizinga ya nyuki na kizifanya kuni" (uk.45).*

Msemo huu *kukata tamaa* unadhihirisha uharibifu wa mazingira ulivyokuwa na athari kubwa kwa wakaazi wa Tikitimaji.

Msemo*" kufa ganzi"* umetumiwa katika ukurasa wa 89, msimulizi Zinji anatumia kurejelea jinsi pua ya Maya wakiwa makao ya Gwadalupe isivyokuwa na makali ya

kunusa harufu yoyote. Maya anawakejeli kwa kusema kuwa ingawa pua zake hazikuwa na makali ya kunusa lakini wao pua zao zilizoea harufu za majalala kule mjini. Msemo huu bado unafafanua suala la uchafuzi wa mazingira na kuelezea hali ya mazingira katika jamii ya Tikitimaji na kule mjini walikotoka hawa vijana.

Katika ukurasa wa 123, msemo *“kutia kitumbua mchanga”.* Sapna anapomweleza ndugu Kikwiro kuwa angependa kuanzisha vuguvugu la kulinda mazingira, anaelezwa kuwa vuguvugu ni hatua ya kuanzisha uhasama wa kisiasa. Mara nyingi viongozi hudhania eti kila vuguvugu linaloanzishwa huwa ni la kijipigia debe la kisiasa. Vuguvugu linaloanzishwa na Sapna si la kisiasa bali ni la kimazingira.

### 4.4.7 Takriri

Takriri ni tamathali ya usemi ambayo huhusu kusisitisa ujumbe ili msomaji apate athari ya msisitizo huo kwa kurudia neno au kifungu cha maneno (Wamitila, 2003). Hivyo takriri huongezea uwiano wa mawazo ya mwandishi na kuyapa uzito fulani.

Katika riwaya ya Tikitimaji, takriri zifuatazo zimejitokeza. Zinji, Sapna, Kombo na Maya waliposhika njia kuelekea Tikitimaji ya upande wa pili kama walivyodokezewa na mama Rehema, waliona tofauti ya uchache wa miti. Kulingana na maelezo ya Rehema palitarajiwa kwamba sehemu hii pangekuwa na miti nyingi. Mwandishi anatumia takriri katika ukurasa wa 18:

*“Hivyo ndivyo alivyosema mama Rehema. Lakini tofauti na alivyosema hapakuwa na miti mingi. Palikuwa na dalili za kukatwakatwa kwa miti. Hapa na pale palikuwa na alama za magurudumu ya magari labda ya lori…. Hapa na pale palikuwa na miti mikavu.(uk.18)*

Urudiaji wa maneno hapa na pale yametumiwa na mwandishi kusisitiza jinsi mazingira yalivyoharibiwa kupitia ukataji wa miti. Jambo hili la ukataji wa miti lilikuwa limeenea

kila pahali. Malori haya yalikuwa yakibeba malighafi ya ujenzi pale mjini. Katika ukurasa wa 19,

*Tulitembea kwa muda kimya kimya. Mara kwa mara tulisikia sauti za bundi waliokuwa wakilia kwenye vichaka vya karibu. Hapa na pale tuliwaona ndege wengine kama visiji, koti na kitwitwi (uk.19).*

Maneno yaya haya '*hapa na pale'* yametumi*wa* na mwandishi kuonyesha uhaba wa viumbe asili hawa. Katika nadharia ya uhalisia, mhimili mojawapo uliongoza utafiti huu ni kuwa: mtunzi anaangalia tatizo na kuchunguza chanzo chake. Kupitia mbinu hii, mwandishi anasisitiza chanzo cha kupungua kwa miti ambacho kilichotokana na ukataji wa miti iliyokuwa inabebwa na malori. Pia hali hii ya ukosefu wa miti inachangia kupungua kwa viumbe asili ambavyo makao yao ni miti. Hii ndio sababu anasisitiza maneno *hapa na pale* ili kuonyesha matokeo ya athari ya ukosefu wa miti kwa viumbe ambao wanategemea miti kama makao yao.

Mbinu hii ya takriri pia imejitokeza katika uk wa 37. Mzee Jududi anapowasimulia vijana hawa kuhusu kilichowapata watu wa Tikitimaji. Anaeleza jinsi watu wa hapo jadi walivyoishi kwa amani na kutunza msitu wa Trimacho ambao ulikuwa rasilimali yao. Anasema kuwa msitu huo ulihodhi kila aina ya miti adimu. Msitu huo ulikuwa chanzo cha miti mingi. Lakini hali hii inabadilika:

'*Akapunua na kuendelea"lakini siku moja, walifika watu*...katika aya ya mwisho, " *ndiyowalifika watu!" akayakariri maneno yake* (uk.37).

Maneno haya yamerudiwa na mzee Jududi kusisitiza athari ya matendo ya watu waliowasili kwa mazingira. Hawa watu ndio waliokuwa wamepewa umiliki wa mlima Trimacho na kuwafurusha wenyeji.

Maneno hapa na pale yamerudiwa katika ukurasa wa 110.

*"Kipepojimbi ilikuwa sehemu tambarare. Palikuwa na uwanja mkubwa wenye nyasi fupifupi, wenye miti kadha hapa na pale iliyojenga bustani yenye nyasi za kijani kinachofifia" (uk.110).*

Uwanja wa Kipepojimbi umefafanuliwa kuwa na nyasi fupifupi na wenye miti kadha hapa na pale. Yalionekana kama yanayofifia. Uwanja wenyewe tunaambiwa kuwa ulikuwa na uchafu wa hapa na pale. Maneno haya; hapa na pale yanasisitiza maudhui ya uharibifu wa mazingira na kuadimika kwa viumbe asili. Mbinu hii ya takriri inatoa msisitizo pamoja na kuonyesha hali halisi ya mazingira kama usemavyo muhimili wa a) wa nadharia ya uhalisia kwamba kazi ya msanii inapasa kuwasilisha ukweli kama ulivyo katika mazingira yake. Kama anavyosema Greg (2004), kwamba kinachomtia ari mwandishi wa fasihi ekolojia ni hatua za kuzoa uhalisia wa dhana za kimazingira.pia mhimili wa b) wanadharia ya uhalisia ambao ulihalisi fasihi kueleza ukweli wa mambo unadhirika.

### 4.5 Matumizi Ya Lugha Katika kuwasilsha masuala ya mazingira katika Riwaya Ya Msimu Wa Vipepeo

#### 4.5.1 Mbinu Rejeshi

Kupitia mbinu rejeshi kanda anakumbuka matukio ya uchafuzi wa mazingira. Katika ukurasa wa 109,

*"…aliweza hata kukumbuka wakati fulani ambapo chama cha wanamazingira kilijaribu kuwapeleka wenye viwanda maakamani. wanachafua maji; wanayaharibu mazingira yetu, walisema. Lakini mahakama iliyohusika ilifutilia hiyo kesi mbali kwa kusema kuwa hapakuwa na ushahidi wa kisayansi wa kutosha."*

Kanda anakumbuka wakati chama cha wanamazingira kilipojaribu kuwapeleka wenye viwanda mahakamani kwa madai kuwa walikuwa wamechafua jiji. Mahakama nayo ikafutilia kesi hiyo mbali kwa madai kuwa ilikosa ushahidi wa kutosha na la mno ni

kuwa kesi ile ilikosa ushahidi wa kisayansi. Katika muktadha huu, mahakama iliathiriwa kisiasa katika shughuli nzima ya kusuluhisha kesi hiyo. Mahakama kama sauti ya mazingira ilipaswa kutoa hukumu kuhusu wale walioharibu mazingira ilizima haki ya mazingira. Ni kupitia mahakama ndipo vitendo viovu vya binadamu kuhusiana na mazingira huzimwa. Hii ndio sauti inayopewa mahakama kama sauti ya mazingira.

Katika ukurasa wa 110, mbinu hii bado inatoa maudhui ya mazingira. Kanda anakumbuka jinsi chama kiki hiki cha mazingira kilivyohimiza waendeshaji magari waache kutumia dizeli ya kawaida na kutumia aina ya dizeli ambayo haina salfa. Kanda anakumbuka haya yote na pia anakumbuka uamuzi wa watu kuhusiana na mapendekezo hayo ya wanachama wa mazingira. Maamuzi yao yaliafikana na maoni ya Reuveny (2007), ambaye alisema kuwa adinasi huliangalia suala la mazingira katika njia tatu. Mmojawapo wa njia alizoorodhesha ni maamuzi ya binadamu kukaa sehemu chafu bila kuleta mabadiliko yoyote. Mawaidha haya ya chama cha wanamazingira yalipuuzwa na wananchi hawa ndiposa hali haikuwa imebadilika kutokana na mpito wa wakati kama alivyokuwa akikadiria mhusika huyu Kanda.

**4.5.2 Nidaa**

Katika ukurasa wa 16, mbinu hii imetumikia ifuatavyo.

*"...kilimo walichokijua kama njia pekee ya kuzumbua riziki hutegemea mvua ambayo haiishi kuwapiga chenga kila wakati; hutokea mawingu mbali huko yakawapa matumaini wakatabasamu na kuanza kuzungumzia kwa msisimko mkubwa kabla ya upinde wa mvua kutokeza na kuwaacha wakimaka, Ahaa!"*

Mbinu hii imetumika kuonyesha athari ya mabadiliko ya hali ya anga kwa maisha ya binadamu. Kulingana na majira ya wanakijiji hawa ulikuwa msimu wa kupanda lakini mambo yalikuwa tofauti.

Uhasama kati ya wanyama na binadamu unajitokeza kupitia mbinu hii ya nidaa katika ukurasa wa 27. Nidaa nyanya! Imetumika na Ndumi kuonyesha kufaidhaika kwake na yale majibwa yaliomuua nyanyake. Ma'Kache alikuwa kwenye ua akiota jua kabla ya kuvamiwa na majibwa wa kijerumani. Majibwa haya yalikuwa yamekosa chakula kwa masaa machache.

### 4.5.3 Uhaishaji

Mbinu ya uhaishaji imetumika katika ukurasa wa 110:

> *"Aliyaelekeza macho yake huko huko na kuona moshi huo wa kafara ukipanda juu. Moshi ambao ulikuwa unatangaza kifo cha mazingira ya jiji."*

Kanda alikuwa akikadiria matatizo ya jiji ya kimazingira yaliyosababishwa na kupuuzwa kwa ushauri uliotolewa na wanamazingira. Tashihisi 'moshi kutangaza kifo cha mazingira ya jiji' imetumiwa na kanda baada ya kuelezea njia mbadala zilizopendekezwa na chama cha wanamazingira za kukabiliana na uchafuzi wa mazingira. Chama hiki kilipendekeza waendeshaji magari kutumia mafuta ya dizeli ambayo haina salfa. Kwa mujibu wa ushauri uliotolewa hamna aliyejali wala kuusikiliza ushauri ule. Basi ni kutokana na vitendo hivi ndipo Kanda anatumia mbinu hii kuonyesha jinsi uhai wa mazingira ulivyokatizwa. Mwandishi huangalia majanga ya kimazingira na kutoa simulizi ya za chanzo cha majanga hayo. Hii ni kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya uhalisia. Kwa kweli mhusika kanda anelaezea asili ya kuwepo kwa moshi ule mrefu jijini. Kupitia mbinu hii

### 4.5.4 Kejeli

Mbinu hii pia imetumiwa na msanii kudhihirisha maudhui ya mazingira. Katika ukurasa wa 99, Julia alishangaa kuona mumewe akitoa kitambaa mfukoni na kufuta machozi. Machozi aliyokuwa akitumia waziri Mkurutu ilikuwa kejeli kwa umma. Machozi haya yalitokana na tetesi kuwa kulikuwa na meli iliyokuwa imeharibikia baharini na

kumwaga mafuta mengi mle baharini. Alipokuwa anatoa machozi haya aliwakejeli wananchi na kuwahadaa waamini kuwa jambo lile halikutokea. Wataalamu wa ekolojia walidai kuwa mafuta haya yaliyomwagika baharini yalitishia viumbe wa majini. Waziri Mkurutu aliepuka suala hili kupitia machozi kwenye vyombo vya habari ambayo yaliwakejeli waliokuwa wanajua ukweli wa tetesi zile za uharibifu wa mazingira.

**4.5.5 Tashibihi**

Kampuni ya NORAD kutoka Norway ilipokuwa ikichimba chemichemi kusuluhisha tatizo la maji la wanakijiji palitokea chemichemi ya ajabu ambayo imeelezwa ifuatavyo;

*Juhudi hizo zilikatizwa na mlipuko mkubwa ambao ulisababisha michirizi mikubwa ya maji angani (ilikwenda juu mpaka mita sabini)...wizara ya utalii na mazingira ilipata kivutio kingine cha kuwavutia watalii na kuwafanya kuzuzumia pale kama nyuki kwenye mbelewele (uk.23).*

Mwandishi anaendelea kwa kueleza kuwa chemichemi ile ilinasa vichwa vya habari kitaifa na kimataifa. La kushangaza ni kuwa hakuna aliyejali kusuluhisha tatizo la maji la wanakijiji. Mazingira haya mapya yamebainishwa na wingi wa watu walioenda kushuhudia mazingira haya mapya kupitia tashibihi hii. Yalikuwa kivutio kwa jamii ingawa hamna aliyeshughulika kuangalia chanzo cha chemichemi hiyo ya ajabu. Shule ya akina Ndumi iliposikia habari hizi nayo iliandaa kuizuru chemichemi hii. Kwake waziri Mkurutu alionea fahari na kujitapa kuwa mwanawe aende ajionee uongozi wake kama waziri wa utalii na mazingira.

Katika ukurasa wa 14, mwandishi anaeleza kuwa jiji kuu nchini lilikuwa na ukame, anaelezea ukame ule unaoifanya mimea kuonekana kama imepukutwa majani. Mbinu hii inasisitiza athari ya ukame kwa mimea. Kazi ya msanii inapasa kuwasilisha ukweli, hii ni kwa mujibu wa muhimili wa a) wa nadharia ya uhalisia.

### 4.5.6 Mandhari

Katika ukurasa wa kwanza, mandhari anayotuonyesha mwandishi ni mandhari ya mazingira yaliyotunzwa. Mwandishi anasema kuwa harufu ya chavua ya maua, sauti za ndege na mkorogo wa sauti nyingine ulipenya hadi chumbani…. Matawi ya mijakaranda huko nje yalicheza na kupigana pambaja na upepo huo. Katika ukurasa wa 7, mwandishi anaeleza kuwa:

*Baada ya kuacha barabara kuu iliyo na miti ya kila aina; mijakaranda, mitini, mierezi, mibambakofi, miwanzi, miwati, mifuu na mikidu, hali ya hewa ilibadilika, inaingia unyevunyevu na baridi ya kiasi* (uk.7).

Katika ukurasa wa 51, mwandishi anaelezea uzuri wa mazingira yaliyotunzwa. Tunaelezwa kuwa upepo mwanana wa bahari uliwachangamsha wanawarsha wakati wanajadili mikakati ya kuinua na kuimarisha utalii…*walikaribishwa na wakabusiwa mashavu na upepolaini.* Kama anavyosema Wamitila (1999) katika makala *ya place and placelessness in Kiswahili:the role ofsetting in Kiswahili creative,* kuwa inapaswa mtu kusoma mazingira katika mandhari ya matini husika. pia mandhari huweza kuelezea hali ijayo ya mazingira. Picha ya mandhari hapa inatupa inatueleza tofauti iliyopo kati ya mazingira yaliotunzwa nay ale yasiotunzwa.

## 4.6 Kumtathimini mwandishi

Katika riwaya hizi mbili, mwandishi anatuelezea mandhari ambayo yanatoa picha halisi ya maliasili. Mandhari, kama mbinu, imetumika na mwandishi kutuelezea idadi ya viumbe asili, sehemu za dunia, spishi mbalimbali na uzuivu wa uchafuzi wa mazingira. Mwandishi, kupitia riwaya hizi amefafanua aina mbalimbali za uchafuzi wa mazingira. Katika riwaya ya Tikitimaji, ukurasa wa 24:

*Palikuwa na mto. Kutokana na maelezo ya mama Rehema lazima huu ndio mto Unasi. Mti huo haukuwa na maji mengi. Palikuwa na maji kidogo kwenye sehemu ya katikati*

*ya mto. Majabali makubwa yaliyolala kwenye sakafu ya mto wenyewe yalidhihirika waziwazi. Mawili matatu yana mabakabaka hapa na pael, athari za miaka zilizo na maji* (uk.24).

Mwandishi anaendelea kueleza athari ya matendo ya binadamu kwa mto uu huu. Mto huu ulikuwa na mashimo makubwa yaliyotokana na ufukuzi wa mchanga. Kama wanavyosema Glotfelty na Fromm (1996) fasihi mazingira huelezea uhusiano wa fasihi na ekolojia. Wanaendelea kusema kuwa uwanja huu umechanganuliwa kupitia diskosi mbalimbali kuhusu mandhari, spishi za viumbe hai, maliasili na uzuifu wa uchafuzi wa viwandani.

Mwandishi amechanganua dhana hizi za ekolojia katika riwaya hizi mbili. Ametupa picha halisi ya aina ya uchafuzi wa mazingira. Katika riwaya ya *Msimu Wa Vipepeo,* mwandishi anaeleza uchafuzi wa maji katika ukurasa wa 99:

> *Huu ulikuwa wakati mfupi tu baada ya tetesi kuzuka nchini kuwa kuna meli ya mafuta iliyoharibikia karibu na kisiwa cha Kisiwandeo na kumwaga mafuta mengi baharini* (uk.99).

Pia anafafanua athari ya kuchafua maji. Anasema kuwa viumbe wa majini wamo hatarini. Wanaohusika katika uchafuzi huu wanamulikwa na vyombo vya habari pamoja na vyama vya mazingira.

Katika riwaya ya *Tikitimaji*, suala la uchafuzi wa maji pia linajitokeza:

> *"Sasa ni yale yale ya ule mto wa mjini. Viwanda vya mafuta vinayatapika masimbi yao mle. Watu wasiojali wanaumwaga uchafu wao humo," akasema Maya* (uk.89- 90).

Aina ya pili ya uchafuzi ambayo mwandishi alizungumzia ni uchafuzi wa hewa. Anafafanua athari ya hewa iliyochafuliwa katika riwaya hizi mbili. Katika riwaya ya Tikitimaji anaeleza:

*Hewa ya hapa ilikuwa tofauti sana na hewa tuliyoizoea. Ilikuwa na joto Fulani. Unyevu hewa wa eneo hili ulikuwa wa juu. Harufu yake ilikuwa mseto wa vumbi...* (uk.17)

*Ile harufu ilianza wingu dogo la moshi kabla ya kuenea na kupanda vidato vya mnuko. Mnuko huo wa mayai viza ukashadidi kiasi kwamba nilihisi kama anayelazimishwa kuingia chumba kilicho jaa moshi* (uk.88).

Mwandishi analinganua hali ya hewa ii hii katika riwaya hii na mazingira ambamo mna utunzaji ifuatavyo:

*"Tulikaribishwa Quadulupe na ule ubaridi unaosababishwa na miti mingi iliyopazunguka. Ile miti mirefu ilikuwa ikicheza huku na huku kutokana na upepo uliokuwepo. Harufu ya mimea, sauti nzuri za ndege na upepo mwanana vilitupiga pambaja kubwa. Tukahisi kama mtoto aliyebebwa juujuu na mzazi wake anayezunguka huku na kule"* (uk.5).

Mwandishi ameelezea mandhari haya tofauti ili kuacha msomaji ajiamulie ni mandhari yapi yanastahili kwake; kama asemavyo Vasquez (1983), kuwa kazi ya sanaa huathiri watu na inachangia katika kuhimiza au kupuuza dhana zao, maazimio yao na hata maadili yao, na kwamba ina msukumo wa kijamii ambao huathiri watu kwa nguvu zake za kijamii na hata za kiitikadi. Katika riwaya ya ***Msimu Wa Vipepeo***, uchafuzi wa hewa unajitokeza katika ukurasa wa 110:

*Alisimama karibu na dirisha huku macho yake yametekwa na moshi mweusi*

*uliotanda upande wa mashariki* (uk.110).

Mwandishi anafafanua kwamba tatizo hili la uchafuzi wa hewa limekuwepo kwa muda. Kupitia kwa vipengele vya fasihi, mwandishi anapendekeza njia mwafaka za kusuluhisha tatizo hili. Anapendekeza matumizi ya diseli ambayo haina salfa. Pia mwandishi anafafanua athari hasi ya uchafuzi wa mazingira.

Mwadishi anatoa picha halisi ya kupungua kwa idadi ya bioanuai. Katika riwaya hizi mbili. Kupungua kwa viumbe hawa kunatokana na kuharibu mazingira wanamokaa. Idadi hii inakuwa nyingi kwa viumbe ambao wanaishi kwenye mazingira yaliyotunzwa.

*Tulitembea kwa muda kimya kimya. Mara kwa mara tulisikia sauti za bundi*

*waliokuwa wakilia kwenye vichaka vya karibu. Hapa na pale tuliwaona ndege*

*wengine kama visiji, koti na kitwitwi (uk.19).*

*…tangu jadi na asili, jamii yao iliishi kwenye msitu wa Mlima wa Tirimacho.*

*Ulikuwa msitu maarufu na uliokuwa na miti adimu sana-mingine hata*

*Haipatikani sehemu yoyote nchini. …msitu ndio ulikuwa kila kitu chao na walijua*

*jinsi ya kuulinda msitu wenyewe* (uk.37).

Ukombozi wa mazingira unakabiliwa na changamoto nyingi. Hii ni kwa sababu katika uhalisia ni vigumu kumpiga mtu aliye na uwezo kuliko wewe. Makabiliano makali yanazuka kati ya wapenda mazingira na wale wanaopenda kinachotokana na mazingira. Mhimili wa c) wa nadharia ya uhalisia unasema kuwa msanii anaangalia matatizo na kuchunguza chanzo chake. Anachunguza mabadiliko ambayo hutokea kwa kipindi cha

kihistoria na kuyatumia kuyasawiri wahusika wake. Mwandishi amfaulu kuwasilisha picha halisi ambayo hukumba mazingira. Uteuzi wa mbinu mwafaka katika riwaya hizi mbili unashadidia kufaulu kwake.

Athari ya uchafuzi wa mazingira kwa afya ya binadamu na uhasama kati ya binadamu na wanyama ni mambo ambayo mwandishi ameangazia pia. Katika riwaya ya ***Tikitimaji***, mwandishi anatumia hadithi ya jinamizi kuelezea maafa ya ukosefu wa mazingira kwa binadamu na viumbe wengine.

> *Wengine wakasema kuwa jinamizi hilo lilikuwa na uwezo wa kusababisha*
>
> *maafa kama vimbuga na hata ukame mkali* (uk.25).

Matendo ya binadmu yamekashifiwa sana na mwandishi. Anaeleza kuwa mazingira yatakuwa sawa kabisa iwapo mwanadamu hatajihusisha nayo; lakini kwa upande wa binadamu, hawezi ishi bila mazingira. Vitendo vya binadamu ndivyo vinayasonga mazingira:

> *"Hata! Haya ya maji kukauka mtoni tunayasababisha sisi wenyewe!*
> *Vitendo vyetu vinasonga koo mazingira yenyewe! Na tukiendelea hivi*
> *Kiwiliwili cha mazingira kitasakamwa hadi kitoke ngamba"*

Mwandishi anawahimiza wanajamii wote kushirikiana katika harakati za kukomboa na kuyalinda mazingira. Utunzaji wa mazingira unaanza na mtu binafsi. Anavipongeza vyama vinavyoundwa ili kutetea haki za mazingira. Kutumia vipengele vya fasihi, mwandishi amewasilisha uhalisia wa masuala ya mazingira. Kama asemavyo Rueckert (1978), fasihi ekolojia hunuia kuleta mageuzi ya kijamii na mazingira kupitia fasihi.

### 4.6.1 Hitimisho

Sura hii ya nne imeshughulikia uchanganuzi wa data ya utafiti wetu. Nimejadilia suala la uhusika na jinsi wahusika wamasawiriwa na mwandishi ili kuwasilisha masuala ya

mazingira. Mbinu za uandishi pia zimeelezwa jinsi zinnavyowasilisha masuala ya mazingira pamoja na tathmini ya kufaulu kwa kwa mwandishi .

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MATOKEO YA UTAFITI NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa utafiti. Utazingatia madhumuni, matokeo pamoja na mapendekezo ya utafiti. Vile vile inatoa maelezo yz ziada na madhumuni, matokeo pamoja na mapendekezo ya utafiti. Ikumbukwe kwamba katika sura ya pili, tuliangalia kiunzi cha nadharia ambacho kiliongoza utafiti wetu. Tulitumia mihimili yote ya nadharia ya uhalisia na nadharia ya fasihi mazingira. Katika sura ya tatu, tulifafanua njia na mbinu za utafiti. Muundo wa utafiti wetu ulikuwa wa kiuchanganuzi ambapo data ilisanywa kwa matumizi ya orodha ya uchunzaji, ikachanganuliwa kutumia mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo nakuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Sura ya nne nayo imewasilisha matokeo ya utafiti huu. Tumetathimini usawiri wa wahusika, maelezo kuhusu uteuzi wa mitindo ya lugha na tathmini ya kufaulu na kutofaulu kwa mwandishi katika kuwasilisha masuala ya mazingira.

## 5.1 Kuhusu madhumuni ya utafiti

Utafiti huu ulinuia kubainisha nafasi ya fasihi katika kuwasilisha masuala ya mazingira, hili ndilo lilikuwa lengo kuu la utafiti huu. Tulitaka kuonyesha jinsi mwandishi Wamitila alivyowasilisha maudhui haya kupitia vipengele vya fasihi. Katika riwaya ya ***Tikitimaji***, wahusika Zinji, Sapna, Maya na Kombo wamesawiriwa kijamii na kiuchumi katika kuelezea uhalisia wa masuala ya mazingira. Katika safari yao kuelekea Tikitimaji, mwandishi anatupa picha halisi ya maeneo wanamopitia kijiogirafia na kutuonyesha mabadiliko ya anga pamoja na bioanuai. Mwandishi analinganisha na kulinganua mazingira walimotoka na yale walimoelekea. Kupitia mitagusano yao na wahusika wengine, mwandishi anadhihirisha mihemko na mielekeo ya binadamu kuhusu mazingira. Wahusika wamepangwa kulingana na majukumu yao. Kuna wale

watetezi na wakombozi wa mazingira kama kina Kanda, Mzee Kitali katika riwaya ya Msimu wa Vipepeo na Zinji, Sapna, Maya na Kombo katika riwaya ya ***Tikitimaji***. Wahusika hawa wamesawiriwa kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Katika mfumo wa kijamii wahusika wanapaswa kushirikiana ili kuhifadhi na kukemea wachafuzi wa mazingira. Nadharia hii imethibitika kupitia wahusika Zinji, Sapna, Maya, Kombo na Mzee Jududi katika riwaya ya Tikitimaji na Kanda, Mkurutu na Fabio Mkalla katika riwaya ya ***Msimu Wa Vipepeo***. Wahusika katika riwaya hizi mbili wamesawiriwa wakitagusana na mazingira katika hali za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Katika riwaya ya ***Msimu Wa Vipepeo***, Mkurutu anatagusana na mazingira kupitia kilimo lakini ananuia kufaidika kisiasa, ambapo anatumaia cheo alichopewa na wananchi kuhujumu mazingira.

Ingawa yeye ni Waziri wa Mazingira na Utalii hajishughulishihata kidogo na mijadala ibuka kuhusiana na visababishi vya uchafuzi wa mazingira. Tetesi zinapoibuka kwamba ipo meli iliyokuwa inamwaga mafuta kwenye mto, hali iliyotishia viumbe wa baharini, yeye anafutilia mbali zile tetesi. Kwa upande mwingine, Kanda anaendeleza shughuli za uhifadhi wa mazingira katika riwaya hii ya ***Msimu Wa Vipepeo***. Ingawa hana kipato kikubwa anajitolea kuhifadhi mazingira na kuwapa nasaha waliochafua mazingira. Anawahimiza watu hao wafuate ushauri unaotolewa na vyama vya mazingira.

Katika riwaya ya ***Tikitimaji***, wahusika Zinji, Sapna, Maya na Kombo ni vielelezo vya wahusika ambao wanaendeleza shughuli za uhifadhi wa mazingira. Wanaungana kwa pamoja na kuunda kundi la vuguvugu la kulinda mazingira. Hawa ni wahusika vielelezo ambao wanathibitisha kuwa jinsi wanasiasa wanavyotengeneza vuguvugu la kisiasa, basi hata mazingira yasitahili kupiganiwa. Ni wahusika waliochanganywa jinsia na hakuna jinsia iliyopewa jukumu la kuhifadhi mazingirapekee yake bali kila mwanajamii amepewa jukumu hili bila kubagua jinsia.

Mhusika Ndugu Kiwiro amesimamia masuala ya usafiingawajei kile akifanyacho ni kinyume kabisa na cheo alichopewa. Yeye ni mhusika ambaye kabisa anadidimiza shughuli za uhifadhi wa mazingira. Kwake mazingira si muhimu; cha muhimu ni kile kinachotokana na mazingira. Anasema kuwa haijalishi kama binadamu atatia kitanzi mazingira au hata kutoboa utumbo wake; kwake kilicho muhimu ni faida itokanayo na mazingira. Ni mhusika anayeamini kuwa mazingira hayapaswi kuhifadhiwa kwa ajili ya urembo. Ingawa yeye ni msomi, hana maarifa asilia kutokana na umuhimu wa uhifadhi wa mazingira kama mzee Jududi ambaye hana kisomo lakini anayo maarifa asilia kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira.

Madhumuni yetu ya pili yalihusu maelezo kuhusu lugha na mitindo iliyotumika kuwasilisha maudhui ya mazingira. Mbinu ya takriri imetumika kwa wingi kwa mfano katika riwaya ya Tikitimaji mwandishi amerudia maneno haya *hapa na pale* kutoa picha halisi ya mimea asilia katika mandhari aliyokuwa akisimulia. Maneno yaya haya pia yamerudiwa katika kurasa zinazofutia kuelezea uchache wa viumbe asili. Aliteuwa mbinu hii ya takriri kimakusudi kusisistiza na kuonya watu kuhusu uchafuzi wa mazingira pamoja na athari za kutohifadhi mazingira.

Katika riwaya ya ***Msimu Wa Vipepeo*** mwandishi ametumia mbinu rejeshi kimakusudi kuelezea mabadilikio ya mazingira kihistoria. Pia mbinu hii anaitumia kuelezea chanzo cha uchafuzi wa mazingira. Kupitia mbinu hii mhusika Kanda anatueleza chanzo cha kuwepo kwa moshi uliotanda kote jijini. Anaeleza kuwa moshi huo ulitokana na kupuuzwa kwa ushauri uliopewa na wanachama wa walinda mazingira wa kutumia aina ya mafuta ya gari ambayo haina salfa. Ubinafsi wa wenye viwanda nao uliwafanya kupuuza ushauri huo.

Lengo letu la mwisho lilihusu tathimini ya kufaulu au kutofaulu kwa mwandishi. Mwandishi amewasilisha masuala ya uchafuzi wa mazingira kama vile: umwagaji wa

uchafu kutoka viwandani kwenye mito, ukataji wa miti, ujenzi wa majumba karibu na fuo za bahari, uhasama kati ya wanyama na binadamu, faida za wanyama, ndege, mlima na misitu kwa wanadamu, changamoto zinzohusiana na ukombozi wa mazingira na nafasi ya wajamii wote kuhusiana na suala la kuajibikia mazingira. Pia mwandishi ametoa suluhisho kuhusiana na maeneo ambayo tayari yamechafuliwa. Anashinikiza ushirikiano wa kila mmoja katika kuhifadhi eneo anamosakini. Mwandishi anafutilia mbali dhana potovu kuwa uchafuzi wa mazingira unafanyika tu mijini. Anasema kuwa uchafuzi wa mazingira ni jambo lililoenea kila pahali hata mashambani. Mara nyingi watu wengi hukimbilia vijijini ili kupata hewa safi. Mwandishi amependekeza njia mwafaka za kukabiliana na hewa chafu kwenye miji yetu ambayo huwa na msongamano wa magari.

Anaonya kuwa suala la uhifadhi wa mazingira huenda likawa suala ngumu iwapo wanadamu hawatakuwa na moyo wa kujitolea na kuwaza kama mlima. Kupitia matini hii, mwandishi ana lengo moja ambalo ni kusitisha haribifu wa mazingira. Hii ndiyo maana inayojitokeza katika riwaya hizi mbili; amehusisha vyama kama vile cha *Enviromental climate Watch* katika riwaya ya ***Msimu Wa Vipepeo*** na chama cha WAZALIMA katika riwaya ya Tikitimaji.

Ingawa kwenye riwaya ya Msimu wa Vipepeo sheria zile hazikutumika kama walivypendekeza hawa walinda mazingira, wahusika wanajutia kwa kutozitumia na wakabaki wakijutia. Hivyo msomaji ameachiwa uamuzi wa kuzifuata ili kuepuka majanga ya kimazingira au kujipata kwenye simanzi ileile. Pia anawahamasisha wanajamii kuhusu uhifadhi wa mazingira kuwa ni wajibu wa kila mwanajamii kupitia vipengele vya fasihi ambayo ni wahusika, mtindo na mandhari.

### 5.3 Mapendekezo kuhusu utafiti zaidi

Masuala ya mazingira yanaendelea kuzungumziwa katika nyanja mbalimbali. Fasihi nayo haijaachwa nyuma katika mjadala huu. Fasihi ya Kiswahili inayouwezo wa kuyamulika masuala ya kiekolojia kama yanavyoonekana katika jamii. Ni muhimu isemwe bayana kuwa vipengele vyote vya fasihi havikushughulikiwa katika utafiti huu. Kwa ajili hii mtafiti anapendekeza utafiti wa baadaye utumie nadharia nyingine kama vile nadharia ya kibaada ukoloni katika kuhakiki masula ya kimazingira kwani ukoloni umechangia pakubwa katika uchafuzi wa mazingira. Hata hivyo, utafiti huu ulijikita kwenye utanzu wa riwaya wa fasihi andishi tanzu zingine za fasihi simulizi zaweza taftiwa.

## MAREJELEO


Barry, P. (1995). *Beginning Theory: An introduction to literary and cultural theory*: Manchester, Manchester University Press.

Beak, J, S. choo & Koo, W. (2008). *The enviromental consequences of globalisation; A Country-Specific Time-Series Analysis:* Paper presented at the American Agricultural Economics Association Annual meeting, Orlando, F1, July 27-29, 2008.

Beull, L. (1995). *The Enviromental Imagination: Thoreau, nature writing, and the formation of American culture*: Cambridge University press.

Cresswell, J. (2009). *Research design: Quantitative, qualitatative mixed method approaches.* Los Angels: SAGE publication.

Dean, J. (2002). *Does trade liliberalization harm the environment?* Anew test. Canadian Journal of Economics 35 (4): 819-842.

Garrard, G. (2004). *Ecocriticism*. London: Routledge publishers., (2007*). Ecocriticism. London:* Routledge publishers

Glotfelty, C. & Harold, F. (1996). *The ecocriticism reader*: Landmarks in Literary Ecology. Athens: University of Georgia press.

Greenblatt, S.(1992). *Marvellous Possessions*: *The wonder of the New World*: Chicago University press.

IPCC (2013). Climate change 2013:*The Physical Science Basis.* Contribution of working group 1 to the fifth Assessment Report of the New York,NY,USA: Cambridge University Press. Available:http://www.climatechange2013.org/images/uploads/WGS_AR5_SPM_Bronchure.pdf.

IPCC (2014).Climate Change 2014: *Mitigation of climate of Climate Change workimg group III Contribution to the The Fifth Assessement Report of the Intergovernmental Panel on Climate change.* Cambridge University Press; New York: 2014 chap AnnexII.2 [Google Scholar]

Greenblatt, S.(1992). *Marvellous Possessions: The wonder of the New World*: Chicago University press.

IPCC (2013). Climate change 2013:*The Physical Science Basis.* Contribution of working group 1 to the fifth Assessment Report of the New York,NY,USA: Cambridge University Press. Available:http://www.climatechange2013.org/images/uploads/WGS_AR5_SPM_Bronchure.pdf.

IPCC (2014).*Climate Change 2014: Mitigation of climate of Climate Change workimg group III Contribution to the The Fifth Assessement Report of the Intergovernmental Panel on Climate change*. Cambridge University Press; New York: 2014 chap AnnexII.2 [Google Scholar]

Kimambo, J. (2015). *Kuchunguza matumizi ya lugha katika riwaya za Kiswahili*: Uchunguzi wa riwaya za Vipuli Za Figo na Siri Za Maisha Kifani.Tasnifu ya uzamilii: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (haijachapishwa).

Kitsao, J. (1975). *A Stylistic Approach for the Study of Written Swahili Prose Texts*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Kothari, C. (2008). *Research Methodology, Methods and Techniques.* New Delhi: New *International* (p) Limited.

Krippendorff, K. (2004). *Content Analysis*. An Introduction to its Methodology (2nd ed). California: Sage publications.

*Landmarks in Literary Ecology"*. Athens: University of Georgia press.

Manes, C. (1996). *Nature and Silence* C. Glotfelty and H. Fromm "The *Ecocritical Reader:*

Masebo J. A. & N. Nyangwine (2006). *Nadharia ya Fasihi*. The general booksellers Ltd: Dar es salaam

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard text-books Graphics and Publishing.

Mohamed, M. (2006). "*Mtindo katika riwaya ya Siku Ya Watenzi Wote*", katika kioo cha lugha, juzuu namba 4, Dar es Salaam: TUKI.

Mohamed, S. A (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Moore, N. (2008). *Eco/feminism, non-violence and the Future of Feminism in International Journal of Politics*, 10(3), 282-298 Taylor and Francis group: Routledge

Msokile, M. (1993). *Msingi ya uhakiki wa fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mulila, A. (2005). *Muala na Mshikamano katika Kiswahili*: Umuhimu wake katikaUchanganuzi wa riwaya ya Vipuli Vya figo. Tasnifu ya chuo kikuu cha Nairobi. (haijachapishwa)

Nabeta, S. (2012). *Shifting towards ecological criticism in oral literature*: *An ecoanalysis of the Maragoli songs*. Maseno University web <http//www.academic.edu.com> 29th June 2016.

Njogu, K & Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa kazi za fasihi*. Augustana college: Rock Island

Nwagbara, U. (2010). *Poetics of Resistance*: Ecocritical reading of Ojaide's poems "Delta Blues and Home Songs and Daydream of Ants and other poems". African study monographs.

Onchangu, R. N. (2013). *Mtindo katika riwaya na hadithi fupi za Clara Momanyi:* Tasnifu ya uzamili, chuo kikuu cha Nairobi(haijachapishwa).

Rigby, K. (2007). *Ecocriticism*: introducing ecocriticism at the twenty first centuary. Edingburgh UP.

Rueckert, W. (1978). *Literature and ecology*: An Experiment in Ecocriticism. Iowa State: University Printing Press.

Senkoro, F. E. M. K (1982). *Fasihi*. Press and publicity centre: Dar es saalam.

Vasquez, A. (1983). *Art and Society in Essays in Marxist Aesthetics.* New York: Monthly Review Press.

Wa Mberia, K. (2001). *Bara Jingine*.Mariba publications: Nairobi.

Wafula, R. & Njogu, K. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Sai Industries Limited: Nairobi

Wallace,C.C. (2001). *Wallace's line and marine organisms. The distribution of staghorn corols in Indonsia*: Balkama publishers. Australia.

Wamitila, K.W (2004). *Kichocheo cha fasihi simulizi na Andishi*. Focus publishers.

Wamitila, K.W (2013). *Tikitimaji*. Nairobi: Vide Muwa publishers.

Wanyonyi, A. (2009). *Sintaksia, italiki, lugha ya kitamathali, Tasfida, Ishara za uwashiriaji na masuala balagha katika riwaya ya Nyuso Za Mwanamke*. Tasnifu ya uzamili (haijachapishwa). Chuo kikuu cha Nairobi.

Yang, K. & Miller, G. J. **(**2008). Handbook of Research Methods in Public Admnistration (2$^{nd}$ edition). New York: M. Dekker.

UNCED (1992) Agenda 21 http://sustainable development Retrieved from un.org/content/documents/agendpdf

## VIAMBATANISHO

### KIAMBATANISHO I: ORODHA YA UCHUNZAJI

| | Yaliyoangaziwa | Vigezo | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kijamii | | Kisiasa | | Kiuchumi | | |
| 1 | Usawiri wa wahusika katika kuwasilisha maudhui ya mazingira | | | | | | | |
| | | Methali | Tashihishi | Kinaya | Maswali Balagha | Tashbihi | Istiari | misem |
| 2 | Mitindo iliyotumiwa kuwasilisha maudhui ya | | | | | | | |
| 3 | Kufaulu kwa mwandishi katika kuwasilisha masuala ya mazingira | | | | | | | |

## KIAMBATANISHO II: BARUA YA SHULE

**Mount Kenya University**

SCHOOL OF POSTGRADUATE STUDIES

MAKI/2014/72016

06th July, 2018

*The Director, Research Coordination Division*
*National Commission for Science, Technology & Innovation*
*Utalii House, 8th & 9th Floor*
*P.O Box 30623- 00100*
*NAIROBI*

Dear Sir/Madam,

RE: LUCY ESTHER WESONGA – REGISTRATION NO. MAKI/2014/72016

The purpose of this letter is to introduce the above named student who is pursuing **Master of Arts in Kiswahili** in the Department of **Languages and Humanities** in the **School of Social Sciences.**

The title of her research is *"Nafasi ya Fasihi Katika Kuwasilisha Mausala ya Mazingira Kupitia Riwaya Teule Tikitimaji **(2013)** na Msimu wa Vipepeo (2006) za K.W Wamitila."*

She has been cleared by the University's Ethics Review Committee (Certificate attached) and now has to proceed to the field to collect data for her research between July and **September 2018.**

Any assistance accorded to her will be highly appreciated.

Thank you.

Registrar
School of Prograduate Studies
Mount Kenya University
P. O. Box 342 - 01000, Thika

Mr. Daniel Gatungu
Registrar, School of Postgraduate Studies

Enc.

Main Campus, General Kago Road, P.O. Box 342-01000 Thika. Tel: +254 67 2820 000,
Cell: +254 720 790 796, 0709 153 000
Email:info@mku.ac.ke, Web: www.mku.ac.ke
**Chartered and ISO 9001 : 2008 Certified Institution.**
**Unlocking Infinite Possibilities**

## KIAMBATANISHO III: BARUA KUTOKA KWA ERC

**Mount Kenya University**

**SEPTEMBER 20, 2017**

**Ref. No. MKU/ERC/0536**

CERTIFICATE OF ETHICAL CLEARANCE

This is to certify that the proposal titled **"NAFASI YA FASIHI KATIKA KUWASILISHA MASUALA YA MAZINGIRA KUPITIA RIWAYA TEULE TIKITIMAJI (2013) NA MSIMU WA VIPEPEO (2006) ZA K.W WAMITILA"**, whose Principal Investigator is Ms Lucy Esther Wesonga (MAKI/2014/72016) has been reviewed by Mount Kenya University Ethics Review Committee (ERC), and found to adequately address all ethical concerns.

**Mr Francis W. Makokha**
**Secretary, Mount Kenya University ERC**

**Sign:** ______ **Date:** 20·09·2017

**Prof. Francis W. Muregi**
**Chairman, Mount Kenya University ERC**

**Sign:** ______ **Date:** 22/09/2017

The Chairman
Mount Kenya University
Ethics Review Committee
P. O. Box 342 - 0100, Thika

Main Campus, General Kago Road, P.O. Box 342-01000 Thika. Tel: +254 067 2820 000, Cell: +254 720 790 796
Email: info@mku.ac.ke, Web: www.mku.ac.ke
Chartered and ISO 9001 : 2008 Certified institution.
Scalis altitudines educationis || Scaling the Heights of Education

## KIAMBATANISHO IV: KIBALI CHA UTAFITI

**THIS IS TO CERTIFY THAT:**
***MS. LUCY ESTHER WESONGA***
**of MOUNT KENYA UNIVERSITY,**
**4441-40200 KISII,has been permitted to**
**conduct research in *Kisii County***

**Permit No : NACOSTI/P/18/70529/22751**
**Date Of Issue : 25th May,2018**
**Fee Recieved :Ksh 1000**



**on the topic: *NAFASI YA FASIHI KATIKA KUWASILISHA MASUALA YA MAZINGIRA KUPITIA RIWAYA TEULE TIKITIMAJI (2013) NA MSIMU WA VIPEPEO (2006) ZA K.W WAMITILA***

**for the period ending:**
***25th May,2019***

.............................
***Applicant's Signature***

.............................................
***Director General***
***National Commission for Science, Technology & Innovation***

## KIAMBATANISHO V: ITHIBATI KUTOKA NACOSTI

NACOSTI

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION**

Telephone:+254-20-2213471,
2241349,3310571,2219420
Fax:+254-20-318245,318249
Email: dg@nacosti.go.ke
Website : www.nacosti.go.ke
When replying please quote

NACOSTI, Upper Kabete
Off Waiyaki Way
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI-KENYA

Ref: No. **NACOSTI/P/18/70529/22751**

Date: **25th May, 2018**

Lucy Esther Wesonga
Mount Kenya University
P.O. Box 342-01000
**THIKA.**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on ***"Nafasi ya fasihi katika kuwasilisha masuala ya mazingira kupitia riwaya teule tikitimaji (2013) na msimu wa vipepeo (2006) za K.W Wamitila,"*** I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Kisii County** for the period ending **25th May, 2019.**

You are advised to report to **the County Commissioner and the County Director of Education, Kisii County** before embarking on the research project.

Kindly note that, as an applicant who has been licensed under the Science, Technology and Innovation Act, 2013 to conduct research in Kenya, you shall deposit **a copy** of the final research report to the Commission within **one year** of completion. The soft copy of the same should be submitted through the Online Research Information System.

GKalerwa

**GODFREY P. KALERWA MSc., MBA, MKIM**
**FOR: DIRECTOR-GENERAL/CEO**

Copy to:

The County Commissioner
Kisii County.

The County Director of Education
Kisii County.

Approved upto 25/05/2019

COUNTY COMMISSIONER
KISII COUNTY

National Commission for Science, Technology and Innovation is ISO9001:2008 Certified

## KIAMBATANISHO V: BARUA KUTOKA KWA WIZARA YA ELIMU

# MINISTRY OF EDUCATION

**State Department for Early Learning and Basic Education**

**Telegram: "EDUCATION"**
**Telephone: 058-30695**
**Email address: cdekisii@gmail.com**
**When replying please quote**

**COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION**
**KISII COUNTY**
**P.O. BOX 4499 - 40200**
**KISII.**

**REF: CDE/KSI/RESECH/76**

**Date: 6th June, 2018**

Lucy Esther Wesonga
Mount Kenya University
P.O. Box 342 – 00100
**THIKA.**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION.**

Following your research Authorization vide your letter ***Ref. NACOSTI/ P/18/70529/22751,*** to carry out research in Kisii County, this letter refers.

I am pleased to inform you that you can carry out your research in the County on"***Nafasi ya fasihi katika kuwasilisha masuala ya mazingira kupitia riwaya teule tikitimaji (2013) na msimu wa vipepeo (2006) za K.W. Wamitila",*** for a period ending

***25th May, 2019.***

Wish you a successful research.

For COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
KISII COUNTY
P. O. Box 4499 - 40200, KISII.
Date:........................
Sign:........................

Justice Kemei
For: County Director of Education
**KISII COUNTY.**

## KIAMBATANISHO VI: BARUA KUTOKA KWA SERIKALI

**THE PRESIDENCY**

MINISTRY OF INTERIOR AND COORDINATION OF NATIONAL GOVERNMENT

Telegrams **"KISII COUNTY"**
Telephone: **(058-30237/Fax 30231)**
**Email cckisii2@gmail.com**
When replying please quote,

**COUNTY COMMISSIONER**
**P.O. BOX 590**
**KISII**

**Ref. No:** KSI/CC/9/5 Vol. III (91)
and date

6th June, 2018

**Lucy Esther Wesonga**
Mount Kenya University
P.O. Box 342 – 00100
**THIKA**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Reference is made to your research authorization letter Ref: No. NACOSTI/P/18/70529/22751 of 25th May, 2018 to carry out research on the ***"Nafasi ya fasihi katika kuwasilisha masuala ya masingira kupitia riwaya teule tikitimaji (2013) na msimu wa vipepeo (2006) za K.W.Wamitila."***

You are hereby authorized to carry out your research in Kisii County up to 25th May, 2019.

COUNTY COMMISSIONER
KISII COUNTY

C.M.OMENGE
**FOR: COUNTY COMMISSIONER**
**KISII COUNTY**

**PLAGIARISM REPORT**

NAFASI YA FASIHI KATIKA KUWASILISHA MASUALA YA MAZINGIRA KUPITIA RIWAYA TEULE TIKITIMAJI (2013 NA MSIMU WA VIPEPEO (2006) ZA K.W WAMITILA

ORIGINALITY REPORT

| 7% | 6% | 2% | 5% |
|---|---|---|---|
| SIMILARITY INDEX | INTERNET SOURCES | PUBLICATIONS | STUDENT PAPERS |

PRIMARY SOURCES

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Submitted to University Der Es Salaam<br>Student Paper | 1% |
| 2 | Submitted to University of Nairobi<br>Student Paper | 1% |
| 3 | erepository.uonbi.ac.ke<br>Internet Source | 1% |
| 4 | erepository.uonbi.ac.ke:8080<br>Internet Source | 1% |
| 5 | Submitted to Kenyatta University<br>Student Paper | <1% |
| 6 | www.augustana.edu<br>Internet Source | <1% |
| 7 | www.ascleiden.nl<br>Internet Source | <1% |
| 8 | Submitted to Eiffel Corporation<br>Student Paper | <1% |

| | | |
|---|---|---|
| 9 | repository.out.ac.tz<br>Internet Source | <1% |
| 10 | elibrary.pu.ac.ke<br>Internet Source | <1% |
| 11 | chomboz.blogspot.com<br>Internet Source | <1% |
| 12 | www.kcse-online.info<br>Internet Source | <1% |
| 13 | www.mwalimuwakiswahili.com<br>Internet Source | <1% |
| 14 | www.qucosa.de<br>Internet Source | <1% |
| 15 | ageconsearch.umn.edu<br>Internet Source | <1% |
| 16 | www.litere.uvt.ro<br>Internet Source | <1% |
| 17 | theartsjournal.org<br>Internet Source | <1% |
| 18 | nenothabiti.blogspot.com<br>Internet Source | <1% |
| 19 | www.swahilihub.com<br>Internet Source | <1% |
| 20 | ojs.utlib.ee<br>Internet Source | |

<1 %

21 Yudina, Olga, and Bryan S. R. Grimwood. "Situating the wildlife spectacle: ecofeminism, representation, and polar bear tourism", Journal of Sustainable Tourism, 2015. <1 %
Publication

22 Submitted to University of Southampton <1 %
Student Paper

23 Mutembei, Aldin (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili and Universität Mainz, Insitut für Ethnologie und Afrikastudien). "Kukitandawazisha Kiswahili kupitia simu za kiganjani: tafakari kuhusu isimujamii", Universitätsbibliothek Leipzig, 2012. <1 %
Publication

24 docplayer.net <1 %
Internet Source

25 repository.suza.ac.tz:8080 <1 %
Internet Source

26 Submitted to University of Nottingham <1 %
Student Paper

27 Submitted to Kisii University <1 %
Student Paper